# Nipashe

Jumatatu Januari 13, 2025 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581920 www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0677 020 710 LIKE & FOLLOW Nipashe

epaper.ippmedia.com Nipashe MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii www.ippmedia.com





UKURASA WA 8

**Wazazi** kaya 250 wagoma kuwapeleka watoto wao shuleni

UKURASA WA 16

**Mifugo** yafa kwa kunywa sumu kutoka mgodini



UKURASA WA 17

**Watu 5,000** waathiriwa matumizi dawa za kulevya Zanzibar

**GUARDIOLA: WALKER KAOMBA KUONDOKA MANCHETER CITY** UK. 21

# Utata mwekezaji kutwaa eneo la shule ya umma

• **Yadaiwa** mwalimu mkuu alipoweka zuio, alihamishwa; Kamati ya Shule yashangaa, DED alonga... *Endelea Ukurasa 3*

UKURASA 3

## Kesi 51 za ACT kupinga Uchaguzi wa Serikali za Mitaa leo





Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk Hussein Ali Mwinyi akiwapungia mkono wananchi waliohudhuria kilele cha maadhimisho ya Miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar kwenye uwanja wa Gombani, Pemba jana. Kushoto ni Rais Samia Suluhu Hassan. **PICHA: IKULU**

UKURASA 2

# Mwinyi atoa angalizo wanasiasa, viongozi dini mwaka wa uchaguzi

**MICHEZO** **WACHEZAJI SIMBA WATOA SIRI YA FADLU** UK.24 **MAONI,** UK.6



Mkurugenzi wa Huduma za Tiba Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. John Rwegasha ambaye ameteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Huduma za Tiba Umoja wa Afrika (AU), akiiaga Menejimenti ya hospitali hiyo, mwishoni mwa wiki, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MNH**

MIAKA 61 YA MAPINDUZI

# Mwinyi atoa angalizo wanasiasa, viongozi dini mwaka wa uchaguzi

**Na Rahma Suleiman,** PEMBA

RAIS wa Zanzibar, Dk Hussein Ali Mwinyi amewataka wananchi kushiriki katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu kwa amani na utulivu kwa kuwa tume zote mbili za uchaguzi zimeanza maandalizi ili uchaguzi huo ufanyike kwa misingi ya amani na sheria.

Vilevile, Dk. Mwinyi amesema kuwa ili kufanikisha uchaguzi huo, ni vyema viongozi wa kisiasa, dini na wananchi kudumisha amani ili kuzidi kupiga hatua za maendeleo kwa vizazi vilivyopo na vijavyo.

Alisema hayo jana wakati akizungumza katika kilele cha Maadhimisho ya Miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar kwenye Uwanja wa Gombani, Pemba.

Rais Dk. Mwinyi alisema: "Leo (jana) ni siku muhimu ambapo miaka 61 iliyopita ukurasa mpya ulifunguliwa baada ya viongozi kujitoa mhanga na kufanya mapinduzi.

Alisema siku hiyo ni kumbukumbu ya wananchi wa Zanzibar kujikomboa kiuchumi, kisiasa na kijamii kutokana na madhila yaliyotokana na kutawaliwa.

Alisema kuna wajibu wa kuwakumbuka waasisi wa mapinduzi, akiwamo Hayati Abeid Amani Karume ili kunufaika na hekima na busara zao.

Rais Dk. Mwinyi alisema katika kuadhimisha miaka 61 ya mapinduzi hayo, anajivunia mafanikio yaliyopatikana katika kufikia malengo, ikiwamo kudumisha amani na umoja huku watu wanaishi katika misingi ya usawa na wananufaika na rasilimali na fursa zote zilizopo bila upendeleo.

Alisema serikali imetafsiri dhamira ya mapinduzi kwa kuleta mageuzi ya kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Rais Dk. Mwinyi alisema nchi imepata mafanikio makubwa katika kukuza uchumi kwa kuongeza ukusanyaji mapato na kudhibiti matumizi yake.

Alisema mafanikio makubwa yamepatikana katika kuwawezesha wananchi kiuchumi, kuimarisha miundombinu ya barabara, viwanja vya ndege, bandari, ujenzi wa nyumba za makazi na biashara, uimarishaji miundombinu ya michezo, huduma za afya, umeme, maji, elimu, demokrasia na utawala bora.

Rais alisema ni wajibu kuendelea na umoja na mshikamano kufanya kazi kwa bidii, uadilifu, umahiri na uzalendo ili kuleta maslahi ya nchi kama walivyofanya waasisi wa mapinduzi.

Akitoa salamu za serikali katika sherehe hizo, Mwenyekiti wa Kamati ya Sherehe hizo ambaye pia ni Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, alisema shughuli hiyo ni kubwa kwa maslahi ya Zanzibar na taifa na kumpongeza Rais Dk. Mwinyi kwa kuendeleza sherehe hizo.

Alimpongeza pia Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuletea mafanikio makubwa nchi na kuyatunza na kuyalinda mapinduzi na Muungano wa Tanganyika na Zanzibar.

Alisema shamrashara za miaka 61 ya mapinduzi zilianza Desemba 15 mwaka jana, miradi mbalimbali ya maendeleo ikizinduliwa na mingine kuwekwa mawe ya msingi. Miradi 113 imezinduliwa au kuwekwa mawe ya msingi katika kipindi hicho.

Sherehe hizo za Miaka 61 ya Mapinduzi Zanzibar zilifana kisiwani Pemba, maelfu ya wananchi wakifurika kwenye Viwanja vya Gombani.

**HALI UWANJANI**

Sherehe hizo zilipambwa na burudani mbalimbali za ngoma za asili na gwaride la askari wa vyombo vya ulinzi na usalama pamoja na maonesho maalumu ya kijeshi.

Saa 8:45 alasiri, Rais Dk. Mwinyi aliwasili uwanjani na kupokewa kwa shangwe na nderemo. Kabla ya kuwasili kwake, alitanguliwa na Rais Samia aliyeingia uwanjani huko saa 8:00 alasiri.

Baada ya Rais Dk. Mwinyi kuwasili uwanjani, mizinga 21 ilipigwa na kukagua gwaride na kupokea maandamano ya wananchi.

Sherehe hizo zilihudhuriwa na viongozi mbalimbali wa kitaifa, wakiwamo marais wastaafu wa Serikali ya Zanzibar na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Viongozi hao ni pamoja na Marais wastaafu, Dk. Amani Abeid Karume, Dk. Ali Muhamed Shein, Makamu wa Rais Philip Mpango, Makamu wa Pili wa Rais, Abdulah, Makamu wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman, Makamu wa pili wa Rais mstaafu, Balozi Seif Ali Iddi na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko.

Wengine ni wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Askon, Spika wa Baraza la Wawakilishi, Zuberi Ali Maulid, Mume wa Rais Samia, Hafidh Ameir, wake wa viongozi na viongozi wa vyama vya siasa.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

MKUTANO NISHATI...

# Biteko apata mwarobaini katikakatika ya umeme nchini

**Na Elizabeth Zaya**

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko amesema wizara hiyo kwa sasa inafanya maboresho makubwa katika njia zote za umeme za zamani, ikiamini ndiyo mwarobaini wa kumaliza kabisa tatizo la kukatika kwa umeme nchini.

Dk. Biteko alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki alipozungumza na TBC kuelekea Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika unaotarajiwa kufanyika nchini Januari 27 na 28 mwaka huu.

Alisema kuwa kwa sasa njia zote za umeme nchi nzima zimezidiwa kutokana na maendeleo ya kiuchumi na hivyo kuwa na mahitaji makubwa ya nishati hiyo.

"Ambacho ninaweza kusema ni kwamba, njia zote za umeme nchi nzima zimezidiwa, na hii ni baada ya nchi yetu kuendelea sana kiuchumi na ukitaka kupima tunaendelea kiuchumi, angalia mahitaji ya nishati hasa kwenye matumizi.

"Ninazungumzia kipindi ambacho ni karibu mwaka mmoja peke yake, mahitaji ya juu yalikuwa ni MW 1,410, leo tunazungumzia mahitaji ya juu MW 1,888. Katika historia ya nchi yetu yote, hakuna kipindi ambacho tumekuwa na ongezeko la MW 400 kwa mwaka.

"Yaani nikizungumza MW 400, maana yake unazungumza mradi mzima wa Mtera, chukua na mradi wa Kidatu na mradi mzima wa Hare, yote hiyo ni mahitaji ya mwaka mmoja. Sasa kukatikakatika huko ni lazima kutokee kwa sababu ili tufanye marekebisho ni lazima tuzime umeme," alisema.

Dk. Biteko aliwataka Watanzania wawe na subira katika kipindi hiki ambacho serikali inafanya maboresho hayo makubwa.

"Kwa mfano tunapojenga laini ya kilomita 30 na unahitaji vilevile kubadilisha transfoma, uichaji, uifanyie majaribio na vitu vyote hivyo vya kitaalamu, hiyo ni lazima itokekee, ambacho ninaweza kuwaomba watanzania ni kwamba tuwe na subira kwa sababu wakati wa mgawo tusingeweza kufanya marekebisho yoyote.

"Watuvumilie kwa sababu ni miundombinu ambayo ni mikubwa, inahitaji muda kuijenga, inahitaji fedha nyingi na uzuri ni kwamba serikali imetoa fedha, sisi kazi yetu ni kwamba kila mahali ambapo tunataka watu wapate umeme, waupate," alisema

Dk. Biteko alisema kwa sasa taifa lina umeme wa kutosha na ziada na uzalishaji umepanda kutoka MW 1,470 hadi MW 3,077.

Alisema mpaka sasa katika Bwawa la Nyerere mitambo sita imeshawashwa na mingine mitatu inatarajiwa kuwashwa ndani ya miezi miwili au mitatu ijayo na kukamilisha yote tisa.

"Hali ya upatikanaji umeme kwa kiasi kikubwa ni wa maji ambayo ni zaidi ya asilimia 56, unafuatiwa na umeme wa gesi ambao tuna MW 1,700, kwa ufupi tumepiga hatua nzuri," alisema.

Alisema kwa sasa wanachofanya ni kuimarisha upatikanaji wa nishati hiyo ya umeme kwa watu kwa kufanyia maboresho makubwa njia zote za umeme za zamani.

"Tumeanza kuimarisha upatikanaji wa umeme kwa watu, kuwafikia, kwa mfano njia tulizonazo za kusafirisha umeme, nyingi ni za zamani sana, zimezidiwa na mahitaji ya watu yamekuwa makubwa sana.

"Tunabadilisha laini, tunatoa nguzo, tunaweka nyaya mpya na transfoma kubwa, vituo vya kupozea umeme na vyenyewe tunavipanua zaidi, kituo cha Gongolamboto, Mbagala, Dege na Kipawa ambako kwa kweli tukifanya marekebisho ya vituo hivyo upatikanaji umeme katika nchi hii na kukatikakatika vitaisha kabisa," alisisitiza Dk. Biteko.

# Utata waibuliwa mwekezaji kutwaa eneo la shule ya umma

**Na Paul Mabeja,** BAHI

WAKAZI wa kijiji cha Mayamaya, wilayani Bahi, mkoani Dodoma, wamepinga kumegwa eneo la shule lenye ukubwa wa ekari 27 na kupewa mtu anayetajwa kuwa mwekezaji kama fidia ya kuwajengea shule ya sekondari.

Kutokana na uamuzi huo, mvutano mkali kwa pande tatu kati ya serikali, mwekezaji na wananchi umeibuka baada ya kutolewa kwa ekari hizo 27 za Shule ya Msingi Mayamaya kama fidia ya kujengewa shule ya sekondari ya kijiji hicho.

Baadhi ya wakazi wa kijiji hicho walisema ardhi hiyo ilitolewa kinyemela na kwamba si makubaliano, wakitaka vyombo vya dola kuingilia kati kuchunguza sakata hilo.

Mwishoni mwa wiki, wananchi walijikusanya na kwenda kung'oa alama za mipaka (bikoni) zinazozenga eneo la shule na linalochukuliwa na mwekezaji ambaye anadaiwa kupitisha katapila na kuharibu mazao waliyokuwa wamelima wanafunzi wa shule hiyo.

Shule ya Msingi Mayamaya iliyoko jirani na makazi ya Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango ni miongoni mwa shule chache zenye maeneo makubwa ambayo inakadiriwa kuwa na eneo la ekari 55 walizokuwa wanazitumia katika miradi ya kilimo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Shule, Irene Mwenda, alisema hakuna taarifa za kuchukuliwa eneo hilo, hata anashangazwa kuona mwekezaji kuingiza trekta kuharibu karanga na mazao mengine yaliyopandwa na wanafunzi kwa madai wameingia eneo lake.

Irene alisema shule haina taarifa za kuchukuliwa kwa eneo hilo na kwamba wasingezuia ujenzi wa sekondari hiyo.

Alisema eneo hilo lilichukua mwekezaji huyo ni upande wa barabarani ambako naye anadaiwa kutaka kujenga shule yake binafsi.

"Hivi wapi mliona watu wanafanya mambo kama tuliyofanyiwa sisi watu wa Mayamaya? Wanakaa watu wachache wanakubaliana kuuza eneo la taasisi kwa kisingizio cha kujenga shule ya sekondari wakati kwenye kata hii tunayo shule na hata madarasa hayajai.

"Kibaya zaidi walifanya figisu wakamhamisha aliyekuwa mwalimu mkuu wa hapa ambaye alikuwa anazuia ndipo wakafanikisha lengo lao," alidai Irene. Akizungumzia ujenzi wa shule ya sekondari, mwenyekiti huyo alisema kuwa tangu mwanzo, wananchi walishirikishwa na kutoa nguvu zao katika uchimbaji msingi na kusogeza mchana ndipo wakaambiwa kuna mfadhili amejitolea kujenga shule hiyo. "Lakini bila kushirikishwa kwenye mikutano ya hadhara na hakukuwa na maelezo kwamba mjenzi anachukua eneo la shule kama sehemu ya gharama zake," alisema.

Alipotafutwa na Nipashe kuzungumzia mvutano huo, Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Bahi, Janeth Mayanja, aliomba mwandishi kutafuta ufafanuzi kutoka kwa Mkurugenzi wa Wilaya ya Bahi kwa kuwa yeye hakuwa na taarifa za kina kuhusu mgogoro huo.

Baada ya kutafutwa, Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Bahi, Zainabu Mlawa alikiri kuufahamu mgogoro huo lakini akasema mwekezaji huyo alipewa kihalali eneo hilo la shule kwenye mkutano wa hadhara ili awajengee wananchi shule ya sekondari na baadaye kuikabidhi kwa serikali, jambo alilosema linaendelea kutekelezwa hadi sasa.

Hata hivyo, kauli hiyo ya mkurugenzi inakinzana na uamuzi uliowahi kutolewa na aliyekuwa Mkuu wa Wilaya hiyo, Godwin Gondwe (sasa Mkuu wa Wilaya ya Singida) ambaye aliwahi kusimamisha ujenzi wa sekondari hiyo kwa maelezo kwamba ulikuwa umekiuka taratibu.

Alipoulizwa na mwandishi kuhusu taratibu za utoaji maeneo ya umma, ikiwamo shule -- kwamba zinatakiwa kupitia njia zipi, Mkurugenzi Zaibanu alisema anafuatilia kama kulikuwa na ukiukwaji.

Hata hivyo, alisema hadi wakati huu anachotambua ni mwendelezo wa ujenzi wa shule ya sekondari kama fidia ya mhusika ambaye hakumtaja jina lake, ili alichukukue eneo la shule ambalo walikubaliana na uongozi wa kijiji.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***

# Kesi 51 za ACT kupinga Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kuendelea leo

**Na Mwandishi Wetu**

MASHAURI 51 yaliyofunguliwa na waliokuwa wagombea wa nafasi za uenyekiti wa mitaa, vijiji na vitongoji kupitia Chama cha ACT Wazalendo kupinga mwenendo mzima wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliofanyika Novemba 27 mwaka jana, yanatarajiwa kutajwa leo katika mahakama mbalimbali nchini.

Kesi hizo zilizofunguliwa katika mahakama za wilaya mbalimbali za Tanzania Bara, zimeanza katika hatua ya awali ya kutolewa wito wa mahakama kuwaita wahusika (wajibu mashauri) kwa ajili ya kutajwa na kujibu mashauri.

Wilaya zilizofunguliwa kesi hizo ni pamoja na Temeke, Lindi, Ilala, Momba, Mkuranga, Mafia, Kigoma, Tunduru, Tandahimba, Kilwa na Kibiti.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mwanasheria Mkuu wa ACT Wazalendo, Omar Said Shaaban, aliyotoa jana, leo Januari 13, kesi tatu tofauti zitatajwa katika Mahakama ya Mkuranga, mkoani Pwani chini ya Hakimu Kenedy Mroso.

Katika mashauri yatakayotajwa Mkuranga, mlalamikaji wa kwanza ni Mmembu Said aliyekuwa mgombea wa nafasi ya Mwenyekiti wa Kijiji cha Tambani, akiwashtaki Msimamizi wa Uchaguzi wa Kijiji hicho na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Juma Kizigo aliyekuwa mgombea wa nafasi ya uenyekiti katika kitongoji cha Mkoga kupitia ACT Wazalendo, anawashitaki Msimamizi wa Uchaguzi wa Kijiji cha Mkoga na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kesi ya tatu itakayotajwa kwa Hakimu Mroso, mlalamikaji ni Bakari Mchonjo anayewashtaki Msimamizi wa Uchaguzi Kitongoji cha Mikengeni pamoja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Mwanasheria Mkuu wa ACT Wazalendo, Wakili Omari Said Shaaban, ambaye pia ni Waziri wa Biashara wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, alisema hatua ya kufungua mashauri hayo ni mwendelezo wa dhamira ya Chama cha ACT Wazalendo kupigania demokrasia na haki za wananchi alizodai ziliporwa wakati wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Maisha Bila Makato

azam Pesa

Tuma Pesa Bure

ADA ZA WATEJA

piga *150*08#

| KIWANGO (TSH) | KUTUMA PESA KWENDA AZAMPESA (TSH) | | | KUTUMA PESA KWENDA MITANDAO MINGINE (TSH) | | | KUTUMA PESA BENKI (TSH) | | | KUTOA PESA (TSH) | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | ADA | TOZO | JUMLA | ADA | TOZO | JUMLA | ADA | TOZO | JUMLA | ADA | TOZO | JUMLA |
| 0 - 999 | BURE | BURE | BURE | 8.5 | BURE | 8.5 | 51 | BURE | 51 | 150 | 10 | 160 |
| 1,000 - 1,999 | BURE | BURE | BURE | 12.75 | BURE | 12.75 | 85 | BURE | 85 | 242 | 10 | 252 |
| 2,000 - 2,999 | BURE | BURE | BURE | 29.75 | BURE | 29.75 | 170 | BURE | 170 | 349 | 10 | 359 |
| 3,000 - 3,999 | BURE | BURE | BURE | 38.25 | BURE | 38.25 | 170 | BURE | 170 | 486 | 14 | 500 |
| 4,000 - 4,999 | BURE | BURE | BURE | 57.8 | BURE | 57.8 | 340 | BURE | 340 | 567 | 27 | 594 |
| 5,000 - 6,999 | BURE | BURE | BURE | 68.85 | BURE | 68.85 | 340 | BURE | 340 | 734 | 54 | 788 |
| 7,000 - 9,999 | BURE | BURE | BURE | 153 | BURE | 153 | 340 | BURE | 340 | 822 | 56 | 878 |
| 10,000 - 14,999 | BURE | BURE | BURE | 153 | BURE | 153 | 850 | BURE | 850 | 1,123 | 102 | 1,225 |
| 15,000 - 19,999 | BURE | BURE | BURE | 420.75 | BURE | 420.75 | 850 | BURE | 850 | 1,129 | 195 | 1,324 |
| 20,000 - 29,999 | BURE | BURE | BURE | 420.75 | BURE | 420.75 | 850 | BURE | 850 | 1,254 | 306 | 1,560 |
| 30,000 - 39,999 | BURE | BURE | BURE | 459 | BURE | 459 | 850 | BURE | 850 | 1,575 | 351 | 1,926 |
| 40,000 - 49,999 | BURE | BURE | BURE | 520.2 | BURE | 520.2 | 1,700 | BURE | 1,700 | 2,070 | 419 | 2,489 |
| 50,000 - 99,999 | BURE | BURE | BURE | 573.75 | BURE | 573.75 | 2,380 | BURE | 2,380 | 2,430 | 573 | 3,003 |
| 100,000 - 199,999 | BURE | BURE | BURE | 956.25 | BURE | 956.25 | 2,550 | BURE | 2,550 | 3,285 | 707 | 3,992 |
| 200,000 - 299,999 | BURE | BURE | BURE | 1,224 | BURE | 1,224 | 3,400 | BURE | 3,400 | 4,590 | 821 | 5,411 |
| 300,000 - 399,999 | BURE | BURE | BURE | 1,453.5 | BURE | 1,453.5 | 3,400 | BURE | 3,400 | 5,400 | 838 | 6,238 |
| 400,000 - 499,999 | BURE | BURE | BURE | 1,759.5 | BURE | 1,759.5 | 3,825 | BURE | 3,825 | 5,850 | 982 | 6,832 |
| 500,000 - 599,999 | BURE | BURE | BURE | 1,912.5 | BURE | 1,912.5 | 3,825 | BURE | 3,825 | 6,300 | 1,245 | 7,545 |
| 600,000 - 699,999 | BURE | BURE | BURE | 2,448 | BURE | 2,448 | 3,825 | BURE | 3,825 | 6,750 | 1,532 | 8,282 |
| 700,000 - 799,999 | BURE | BURE | BURE | 3,289.5 | BURE | 3,289.5 | 4,250 | BURE | 4,250 | 6,750 | 1,700 | 8,450 |
| 800,000 - 899,999 | BURE | BURE | BURE | 3,289.5 | BURE | 3,289.5 | 4,250 | BURE | 4,250 | 6,750 | 1,750 | 8,500 |
| 900,000 - 1,000,000 | BURE | BURE | BURE | 4,590 | BURE | 4,590 | 5,100 | BURE | 5,100 | 6,750 | 1,776 | 8,526 |
| 1,000,001 - 3,000,000 | BURE | BURE | BURE | 4,590 | BURE | 4,590 | 5,100 | BURE | 5,100 | 6,750 | 1,875 | 8,625 |
| 3,000,001 - 10,000,000 | BURE | BURE | BURE | 4,590 | BURE | 4,590 | 5,100 | BURE | 5,100 | 7,125 | 2,000 | 9,125 |

| TUKIO | ADA |
|---|---|
| Kuangalia salio/Taarifa ndogo | BURE |
| **TAARIFA YA MWEZI** | **ADA** |
| Mwezi jana/Mwezi huu | BURE |

Hakikisha namba na majina ya mpokeaji kabla ya kutuma pesa.

Hakikisha unatunza namba yako ya siri, usimpe mtu yeyote namba yako ya siri iwe wakala wa Azampesa au mfanyakazi wa Azampesa.

Mteja unaweza kuweka ama kupokea hadi Tsh 10,000,000 kwa siku na unaweza kutuma au kutoa hadi Tsh 5,000,000 kwa siku.

MALIPO YA AZAMPESA

Huduma Za Azam, LUKU, Bili Za Maji, Ada Za Shule, Tiketi za Ndege, Mafuta, Manunuzi, Migahawa, Muda Wa Maongezi, Lipa bili, Hisa, Ving'amuzi Vya TV

MALIPO YA SERIKALI

May 2024

218319301

GET IT ON Google Play

Download on the App Store

Kwa maelezo zaidi juu ya vigezo na masharti ya huduma tembelea tovuti: www.azampesa.co.tz

Huduma kwa wateja, Piga namba 0800 785 555

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

**TANGAZO LA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KATIKA MIKOA YA NJONBE, RUKWA, SONGWE NA RUVUMA KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA ZA NYASA, MBINGA, MJI WA MBINGA, WILAYA YA SONGEA NA MANISPAA YA SONGEA.**

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote kuwa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza na route ya tisa utafanyika katika Mikoa ya Njombe, Rukwa, songwe na Ruvuma katika Halmashauri ya Wilaya za Nyasa, Mbinga, Mji wa Mbinga, Wilaya ya Songea na Manispaa ya Songea tarehe 12 hadi 18 Januari, 2025. Zoezi la uboreshaji wa Daftari litafanyika kwa siku saba kwa kila kituo katika Mikoa hiyo.

1. SIKU: Uboreshaji utafanyika kuanzia siku ya Jumapili tarehe 12 hadi siku Jumamosi tarehe 18 Januari, 2025.
2. VITUO: Uboreshaji utafanyika katika vituo vilivyomo katika Mitaa, vijiji na vitongoji.
3. MUDA: Vituo vitafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni

**Uboreshaji utahusisha: -**

1. Kuandikisha Wapiga Kura wapya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa miaka 18 na zaidi ambao hawakuwahi kuandikishwa hapo awali, na ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka
2. Kuboresha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine la kiuchaguzi (Jimbo au Shehia).
3. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika.
4. Kuboresha au kurekebisha taarifa za wapiga kura.
5. Aidha,Wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa zao na wanaohama kituo cha kupigia kura au vyote viwili kwa pamoja, wanaweza kuanzisha mchakato wa kuboresha kwa kujaza fomu maalum kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Tume www.inec.go.tz au anuani ya ovrs.inec.go.tz kwa kujaza namba ya kitambulisho cha Taifa, namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu ya mpiga kura na jina la shehia anayokusudia kuhamia, kisha watapokea ujumbe wenye namba ya utambulisho (token number) ambayo watakwenda nayo katika kituo cha kuandikisha Wapiga Kura ili kukamilisha taratibu na kupatiwa kadi ya mpiga kura.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kuandikishwa itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika katika kituo cha kujiandikisha atachukuliwa alama za vidole vyote kumi vya mikono na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni.
- Ni muhimu kujiandikisha sasa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili uweze kupiga kura ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na chaguzi zijazo.
- Mpiga Kura ambaye ana simu ndogo (maarufu kama kitochi au kiswaswadu) anaweza kuingia kwenye mfumo wa OVRS kwa kupiga *152*00#, kisha, atachagua namba 8 na kubonyeza, kisha atachagua namba 2, kisha atabonyeza namba 3 hapo atapata huduma namba moja hadi nne. Atachagua huduma anayoitaka kati ya hizo nne. Hatimaye, atapata namba ya utambulisho (token number) atakayokwenda nayo kituoni kukamilisha mchakato wa kupata kadi ya mpiga kura.
- Mpiga kura anaweza pia kuwasiliana moja kwa moja na Maafisa wa Tume waliopo katika Kituo cha Huduma kwa Mpiga Kura kwa kupiga simu namba 0800112100 bila malipo.
- Zoezi hili halitawahusu wapiga kura ambao waliandikishwa awali na hawajahama maeneo yao ya kiuchaguzi na wana kadi zao za mpiga kura.

**KUJIANDISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA**

Limetolewa leo tarehe 03 Januari, 2024 na:

**Kailima, R. K**
**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**



Mbunge wa Ushetu Emmanuel Cherehani (Katikati) akizungumza na viongozi wakati wa harambee ya uchangiaji wa ujenzi wa bweni la wanafunzi wa kike sekondari ya Chona Halmashauri ya Ushetu-Kahama juzi. Kushoto kwake ni Mkuu wa Divisheni Elimu Sekondari Emmanuel Malima na kulia ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi(CCM) mkoa wa Shinyanga, Mabala Mlolwa jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Mkurugenzi wa Tiba Muhimbili ateuliwa kuongoza kamisheni AU

**Na Christina Mwakangale**

MKURUGENZI wa Huduma za Tiba Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. John Rwegasha ameteuliwa kushika wadhifa wa Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Tiba, Kamisheni ya Umoja wa Afrika (AU) baada ya kuwashinda washindani wengine kutoka nchi saba za barani humo.

Makao Makuu ya kamisheni hiyo yako Addis Ababa, Ethiopia. Dk. Rwegasha anatarajiwa kuanza rasmi kazi mwezi ujao.

Akizungumza na Menejimenti ya MNH mwishoni mwa wiki hii, mbali na kuwaaga watumishi wa MNH, Dk. Rwegasha alisema anamshukuru Mungu kwa nafasi hiyo ambayo ilikuwa na ushindani mkubwa.

Alisema kuwa katika mchakato wa usaili, amefanikiwa kufaulu na hatimaye kuteuliwa rasmi, akiwashinda washindani wenzake katika nafasi hiyo kutoka mataifa saba ya Afrika.

Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Prof. Mohamed Janabi, akimpongeza Dk. Rwegasha, alimtakia kila la kheri na uwakilishi mzuri kwa Tanzania katika kutekeleza majukumu ya chombo kikubwa cha AU, hususani eneo la sekta ya afya barani.

Dk. Rwegasha ni Bingwa Mbobezi wa Magonjwa ya Mfumo wa Chakula na Ini. Kwa jitihada zake alifanikisha MNH kuanzisha kituo cha utoaji mafunzo na tiba ya magonjwa hayo nchini mwaka 2013.

Baadaye alichaguliwa kuwa Mkuu wa Kitengo cha Magonjwa ya Mfumo wa Chakula na Ini hadi 2018 alipoteuliwa kuwa Mkuu wa Idara ya Magonjwa ya Ndani yenye vitengo 11 na baadaye Oktoba 2022, aliteuliwa kuwa Mkurugenzi wa Huduma za Tiba MNH, akisimamia idara saba.

Kuhusu elimu yake, Dk. Rwegasha ana Shahada ya Kwanza ya Udaktari ya Chuo Kikuu cha Makerere (Uganda); Shahada ya Uzamili ya Udaktari ya Chuo Kikuu cha Aga Khan (Kenya); Shahada ya Uzamili ya Sayansi katika Uongozi ya Chuo Kikuu Mzumbe; Stashahada ya Usimamizi wa Afya ya Chuo Kikuu cha Washington, Marekani. Dk. Rwegasha kitaaluma ni mtaalamu wa tiba, akisoma kutoka vyuo vikuu tofauti pamoja na vya Uingereza na Afrika Kusini.

# Mifumo uuzaji mazao yamkuna Shigela

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

MKUU wa Mkoa wa Geita, Martin Shigela amesema mifumo ya uuzaji mazao ya nafaka na mazao mchanganyiko itaimarisha ukuaji wa sekta ya kilimo na kumlinda mkulima dhidi ya unyonyaji kwenye bei na vipimo.

Shigela alisema hayo mjini hapa mwishoni mwa wiki iliyopita baada ya kukutana na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA), Irene Mlola wakati wa ziara yake ya kikazi katika mikoa ya Kanda ya Ziwa.

Alisema Geita inaunga mkono juhudi zinazofanywa na serikali kupitia COPRA katika kurasimisha biashara ya nafaka na mazao mchanganyiko kwa kuweka mazingira ya kuhakikisha mkulima ananufaika na kazi ya mikono yake.

"Geita tunaunga mkono jitihada za Serikali kupitia COPRA, hivyo tutaendelea kushirikiana ili kuhakikisha wakulima wananufaika na uwepo wa mamlaka hiyo,"alisisitiza Shigela.

Alisema wao kama serikali ya mkoa watatoa ushirikiano kwa maofisa wa COPRA katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku mkoani Geita.

Aliwataka wakulima na wafanyabiashara wa mazao wa Geita kutoa ushirikiano kwa maofisa COPRA watakapohitajika.

Kwa upande wake, Irene, alisema mamlaka hiyo imeanza kuweka wataalamu wake watakaoshirikiana na wengine mikoa ya kanda hiyo kuhakikisha biashara ya nafaka na mazao hayo inafanyika kwa kufuata mifumo ilivyoelekezwa na serikali.

Alisema wataalam hao watafanya kazi kwa kuhakikisha mazao yote yanayozalishwa katika mikoa hiyo yanakuwa na ubora wa hali ya juu unaohitajika katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

Irene, alimshukuru Shigela kwa ushirikiano aliowapa na kusisitiza COPRA italeta mageuzi makubwa kwa wakulima na kunufaika kiuchumi.

Alisema atahakikisha wataalam wa COPRA wanafanya kazi kwa weledi kwa kushirikiana na wataalam wa sekta ya kilimo kuanzia ngazi ya vijiji hadi mkoa na kuleta matokeo chanya kwa wakulima na taifa.

Mkurugenzi huyo wa COPRA anaendelea na ziara ya kikazi katika mikoa hiyo baada ya kukamilisha baadhi ikiwamo Simiyu, Kagera na Geita.

Ziara hiyo ina lengo la kutambulisha mamlaka hiyo, mkurugenzi huyo, maofisa wake na kuweka mazingira ya utendaji kazi wa pamoja ili kuendesha shughuli za biashara ya nafaka na mazao mchanganyiko yanayolimwa huko.

# Wadau wa maendeleo wasisitiza uzingatiaji afya ya uzazi dira 2050

**Na Maulid Mmbaga**

WADAU wa maendeleo wa kimataifa wametoa wito kuongeza msisitizo kwenye afya ya uzazi, vijana balehe, watoto na kuweka mikakati madhubuti ya kupunguza utapiamlo nchini, wakitaka iwe mojawapo ya nguzo katika Rasimu ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

Akizungumza wakati wa programu ya ushirikiano na washirika wa maendeleo iliyofanyika juzi mkoani Dar es Salaam, Naibu Mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA), Melissa McNeil-Barrett, alisisitiza umuhimu wa masuala ya afya katika kufanikisha maendeleo endelevu na jumuishi.

Katika hotuba yake, McNeil-Barrett alieleza kuwa suala la idadi ya watu linahusiana moja kwa moja na uwekezaji katika afya bora ya vijana na elimu itakayosaidia kuchochea maendeleo ya kijamii na taifa kwa ujumla.

"Ni muhimu kuhakikisha wanawake wanapata fursa za kupanga familia zao kwa ufanisi, jambo ambalo linasaidia kupunguza viwango vya uzazi na kuongeza nafasi ya kizazi kinachofuata kufikia uwezo wao kamili," alisema.

McNeil-Barrett pia alisisitiza uwekezaji katika afya ya uzazi na kinga dhidi ya magonjwa yasiyo ya kuambukiza, ni sehemu muhimu ya kuboresha maisha ya watu na kuhakikisha ustawi wa jamii kwa ujumla.

Pia alibainisha kwamba asilimia 20 ya vifo vya wajawazito vinatokea miongoni mwa vijana, jambo ambalo linahitaji hatua madhubuti kukabiliana nalo na kulikomesha kabisa.

Alihimiza kuwapo msisitizo wa kipekee katika kuhakikisha upatikanaji taarifa na huduma za afya kwa vijana balehe, akisema kuwa hili ni muhimu katika kuzuia changamoto kama mimba zisizotarajiwa na matatizo mengine ya uzazi.

McNeil-Barrett alipongeza serikali kwa juhudi zake katika kuandaa rasimu ya dira hiyo, akieleza kuwa imeweka msingi mzuri wa kushughulikia changamoto za kijamii na kiuchumi zinazokabili taifa, huku akihimiza kufanyika maboresho zaidi katika sehemu zinazohusiana na afya ya uzazi, watoto, na vijana balehe.

Mkurugenzi wa Shirika la Chakula Duniani (WFP) nchini Tanzania, Ronald Tran Ba Huy, alisisitiza umuhimu wa sekta ya kilimo kuweka ulinzi wa kijamii na mikakati ya kupunguza utapiamlo kama maeneo muhimu ya kuimarishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

Alieleza kuwa sekta ya kilimo ina mchango mkubwa katika ajira za vijana na ukuaji wa uchumi wa ndani na kikanda.

"Tanzania tayari ni kapu la chakula kwa ukanda huu, lakini inaweza kuwa kapu kubwa zaidi. WFP inanunua bidhaa nyingi za ndani kwa ajili ya shughuli zake za kikanda, na hivyo kuna fursa kubwa ya kukuza sekta hii," alisema Ronald.

Kuhusu mabadiliko ya tabianchi, alisisitiza haja ya kujumuisha miradi ya kukabiliana na maandalizi ya majanga kwenye sera za maendeleo.

"Hatuongelei tu miundombinu mikubwa, bali pia miradi ya kijamii na maandalizi kwa ajili ya changamoto zinazotokana na tabianchi," alisema.

Ronald pia aligusia umuhimu wa kuimarisha mifumo ya hifadhi ya jamii ili iweze kukabiliana na majanga, akieleza kuwa mifumo hiyo inapaswa kuwa na uwezo wa kujibu changamoto za ghafla, ikiwa ni sehemu ya mikakati ya maendeleo.

Hata hivyo, moja ya changamoto kubwa aliyoitaja ni viwango vya juu vya utapiamlo miongoni mwa watoto, akibainisha kuwa hali hiyo inazuia watoto kufikia uwezo wao kamili.

"Tutafurahi kushirikiana nanyi kuhakikisha kuwa suala la kupunguza utapiamlo linapewa uzito katika dira hii," alisema Ronald.

TANGAZO

# ZIPA MHIMILI WA UWEKEZAJI BINAFSI ZANZIBAR

**Na Mwandishi Wetu**

UWEKEZAJI katika sekta yoyote ni mhimili mkubwa katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika jamii na taifa lolote duniani. Uwekezaji huchochea ukuaji wa uchumi na kuongeza uzalishaji wa bidhaa kwa ajili ya mauzo ya ndani na nje, ajira kwa wananchi na ongezeko la mapato ya serikali kupitia kodi mbalimbali na mauzo ya bidhaa.

Katika kutambua hilo, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) iliandaa mipango mbalimbali kwa ajili ya uwekezaji ili kuinua uchumi wa visiwa hivi na maendeleo endelevu katika nyanja mbalimbali. Matokeo ya mipango hiyo yanaonekana sasa wakati Zanzibar inatimiza miaka 61 ya Mapinduzi.

"Kutokana na umuhimu wa Uwekezaji nchini, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanya mabadiliko mbalimbali hadi kufikia 2023, Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar imepata Sheria mpya namba 10 ya 2023 iliyoufanya uwekezaji kukabiliana na mabadiliko ya kiuchumi Duniani kwa kutoa fursa ya moja kwa moja kwa mgeni kumiliki asilimia 100 ya Uwekezaji Zanzibar.

"Lengo ni kuhakikisha kunakuwa na uwekezaji wenye mafanikio na kuleta maendeleo endelevu," anasema Mkurugenzi Mkuu wa ZIPA, Saleh Saad Ahmed alipohojiwa kuhusu hatua zilizofikiwa Zanzibar kuchochea Uwekezaji.

Saleh anabainisha kuwa uwekezaji ndiyo Mhimili mkuu katika maendeleo ya taifa lolote Duniani ikiwemo Zanzibar. Anasema awali watalii wengi walikuwa wakienda Mombasa katikati ya miaka ya 2000, hali ilibadilika na Zanzibar kuchukua nafasi.

"Mapinduzi yalikuja kuleta utawala bora na kuangalia nini hatma ya Zanzibar kiuchumi kwa miaka inayofuata. Viongozi waliotangulia kabla ya Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi walianzisha mambo ambayo yameleta mafanikio makubwa kiuchumi Zanzibar. Rais Mwinyi ameendeleza zaidi na kuna matokeo makubwa katika ukuzaji uwekezaji na maendeleo kwa ujumla," anasema.

Mkurugenzi huyo anabainisha kwamba Zanzibar, uwekezaji umechangia ukuwaji wa sekta hiyo,



*Mkurugenzi Mtendaji Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) Nd. Shariff Ali Sharif*

kutokana na kuwepo uwekezaji mkubwa wa mahoteli na nyumba za makaazi jambo ambalo limechangia kukuza sekta ya Utalii Zanzibar kwa asilimia 25 Hadi 30

Kwa mujibu wa Saleh, kati ya miradi 1,255 iliyosajiliwa ZIPA, 600 ni ya hoteli kwa maana ya huduma za malazi na chakula na kwamba katika uongozi wa sasa wa Dk. Mwinyi kumekuwa na kasi kubwa katika usajili wa miradi ya uwekezaji.

"Katika Uongozi wa Rais Dk Mwinyi miaka minne ZIPA imesajili miradi yenye thamani ya Dola bilioni 6,065,009,035 za Marekani. Kabla ya hapo hakuna mwaka ambao iliwahi kusajiliwa Zaidi ya miradi 50.

"Katika kipindi cha Dk. Mwinyi, miradi isiyopungua 420 imesajiliwa Zanzibar na kutoa ajira zaidi ya 20,000" anasema.

Anaongeza kuwa: "Kabla ya Mapinduzi hakukuwa na maendeleo kama haya au manufaa kwa wazawa. Lakini kwa sababu ya sheria na katiba zetu katika kuwajali wananchi, kumekuwa na mafanikio haya. Hata ongezeko la idadi ya watu linaonyesha kuwa Zanzibar panafaa kwa uwekezaji kwa sababu pana utulivu."

Kuhusu maendeleo kisekta, anasema uwekezaji mkubwa umefanyika katika miradi ya hoteli kwa sababu ya ongezeko la watalii. Kwa sasa anasema kuna wastani wa watalii 600,000 wanaoingiza Zanzibar kwa mwaka na hoteli zilizoko ni 3,157.

Sababu kubwa ya ongezeko hilo, anasema ni sera na mikakati bora ya serikali katika kukuza uwekezaji katika sekta mbalimbali, utalii ukiwamo. Anasema sera hizo na sheria zimesababisha kutokuwapo kwa udhalilishaji dhidi ya wageni na wazawa na vitendo kama hivyo vikiripotiwa na kubainika ni kweli, mtu anachukuliwa hatua mara moja na kama ni mtalii au mgeni, anaondolewa mara moja.

**SEKTA YA MILKI**

Kutokana na wimbi la uwekezaji kuwa kubwa Zanzibar, Saleh anasema kumekuwa na kasi katika maendeleo ya sekta ya makazi hivi sasa. Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, hivi sasa kuna miradi 114 ya uwekezaji katika sekta hiyo imeandikishwa jambo linalodhihirisha kuwa kuna umuhimu wa kuwekeza katika eneo hilo.

Anasema katika kuwavutia wawekezaji wa sekta hiyo, mtu anayeuza nyumba yenye thamani ya Dola za 100,000 za Marekani anapata hati ya ukaazi kwa kipindi cha miaka miwili na haruhusiki kuifanyia biashara. Pia watu wanashajihishwa kutokufunga nyumba wanapoondoka bali wakodishe ili kodi za serikali ziendelee kulipwa.

"Katika hili lengo tunataka kuifanya Zanzibar kuwa sehemu ya pili ya ukaazi kwa watu (second home) kama ilivyo Dubai. Mtu ana nyumba Dubai na sehemu nyingine, ndivyo tunavyotaka Zanzibar iwe," anasisitiza.

Alisema kupitia njia ya mfumo wa kielektroniki anapata cheti kupitia mtandaoni na malipo anafanya kwa njia ya mtandao. Tayari maombi 90 yamefanyika na wawekezaji wamepata vyeti kwa njia ya mtandao. Mfumo huu pia unaokoa muda ma fedha.

"Kupitia mfumo huu wa Zanzibar Investment Electronic Window (ZIEW) masuala yote yamefungamanishwa pamoja yakiwamo uhamiaji, ardhi. Katika kutoa huduma bora, kimeanzishwa kituo cha huduma kwa pamoja ambacho kinahusisha uhamiaji, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA), Wakala wa Majengo (ZBA), utalii, mazingira na watu wa ardhi," anasema.

MAGEUZI MAKUBWA

Tangu ilipokuwa Idara ya Uwekezaji chini ya Wizara ya Fedha na Uchumi mwaka 1986 hadi mamlaka sasa, kumekuwa na mageuzi makubwa katika masuala ya uwekezaji Zanzibar.

Moja ya mafanikio ni kumtambua Mzanzibari na Mtanzania aliyeko ughaibuni (diaspora) tofauti na awali alivyokuwa akionekana mgeni. Pia mabadiliko ya sheria kuhusu uwekezaji yanawataka wawekezaji kurejesha kwa wananchi sehemu ya faida wanayopata (CSR).

Mafanikio mengine ni kuwawezesha wawekezaji kupata ardhi kwa ajili ya kuweka miradi yao pamoja na kupunguza viwango wanavyopaswa kulipa. Viwango hivyo, kwa mujibu wa Saleh, kwa Watanzania vimepungua kutoka Dola 300,000 za Kimarekeni hadi Dola 200,000 na kwa wageni kutoka Dola milioni 2.5 hadi Dola 500,000.

Ili kufanikisha azma ya uwekezaji, ZIPA imetenga maeneo maalum ya Uwekezaji ikiwemo maeneo Huru na ardhi ya akiba ambayo hutolewa kwa wawekezaji. Baadhi ya maeneo hayo ni Free Economic Zone Fumba (hekta 3,000), Viwanda Vidogo Amani (hekta 12.6), Bandari Huru Maruhubi (hekta 5.6), Micheweni (hekta 808.8), mashamba ya mipira na visiwa kwa ajili ya uwekezaji.

**MIPANGO 2025**

Katika mwaka 2025, ZIPA imepanga kupita mkoa kwa mkoa na vyuo kutoa elimu kuhusu uwekezaji ikiwamo kuwamo kwa kampuni za ndani za ushauri elekezi katika masuala hayo. Pia imepanga kusimamia uwajibikaji wa wawekezaji kutekeleza utoaji wa misaada ya maendeleo ya jamii zilizoko katika maeneo ya uwekezaji (CSR) kulingana na mipango ya mikoa.

"Pia tunataka wananchi watangaze dhamira zao katika uwekezaji. Wengi wanakosa mitaji kwa maana ya fedha na uelewa wa masuala ya uwekezaji. Lengo hapa ni kuhakikisha mwananchi wa kawaida anajumuishwa na kusaidiwa katika masuala ya uwekezaji," anasisitiza Saleh.


SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR

**MAMLAKA YA KUKUZA UWEKEZAJI ZANZIBAR (ZIPA)**

**MAADHIMISHO YA MIAKA 61 YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**



*Dkt. Hussein Alli Mwinyi na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi*






*Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*

Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa MAMLAKA YA KUKUZA UWEKEZAJI ZANZIBAR (ZIPA) Dkt. Hussein Alli Mwinyi na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Dkt. Samia Suluhu Hassan wanaungana na watanzania wote katika sherehe za kuadhimisha Miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar

**1964-2025**

www.zipa.go.tz

# Invest in Zanzibar Now!

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Simba, Yanga kuna mengi ya kujifunza michuano GIFT

**MICHUANO** ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), kwa timu za wasichana chini ya miaka 17 (Girls Integrated Football Tournament- GIFT), Ukanda wa CECAFA, iliyoanza kutimua vumbi nchini tangu Januari 7, inatarajiwa kutamatika Januari 18, mwaka huu, huku timu inayolelewa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), TDS Girls Academy, ikiwa tayari imetinga fainali.

Ilitinga fainali juzi baada ya kuichapa Aigle Noir ya Burundi mabao 2-0, katika mchezo uliopigwa Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam inapofanyika michuano hiyo.

Jumla ya timu nane zinashiriki michuano hiyo. Timu hizo ni Kenya Elite Junior Academy, KAS, JKT Queens, City Lights ambazo zipo Kundi A, na TDS, Boni Consilli Girls, Aigle Noir FC na Hilaad FC, zipo Kundi B.

Ukitazama hapo utagundua kuwa timu nyingi hapa ni za kutoka nje ya nchi, vituo vya michezo, pamoja na shule za sekondari.

Ajabu iliyopo kwenye michuano hii ni kwamba pamoja na kuchezwa hapa nchini, lakini ni JKT Queens ndiyo timu pekee ya Ligi Kuu iliyopeleka timu yake ya vijana kwenye michuano hiyo.

Kwa ujumla tulitarajia kabla ya michuano hiyo, kungekuwa na mashindano ya timu za vijana za U-17 kutoka zile za Ligi Kuu ya Wanawake nchini, Simba Queens, Yanga Princess, Mashujaa Queens, Bunda Queens, Ceasiaa Queens, Alliance Girls, Mlandizi Queens, Get Program, Fountain Gate, Princess na JKT Queens zikichuana vikali ili kuwania nafasi ya kushiriki michuano hiyo ya GIFT.

Kama Klabu ya Aigle Noir, imeweza kumudu kuwa na timu ya U=17 ya wasichana kwa ni nini timu kongwe za soka nchini Simba na Yanga zishindwe? Hii ina maana hazina wachezaji wa umri huo kwenye vikosi vyao zaidi ya vikosi vya wakubwa tu.

Hii haileti picha nzuri kwenye kukuza soka la wanawake nchini, badala yake klabu zetu zinaendelea kutumia na kusajili wachezaji kutoka nje ya nchi na wale wa ndani wengi wakiwa hawajapita njia sahihi ya kulelewa kisoka.

Hapa tunaona nchi kama Kenya na Burundi zimeleta wasichana wao chini ya miaka 17, na nchi hizo zina wachezaji wengi katika klabu za Ligi Kuu soka Wanawake, hivyo wanazidi kujitengenezea mazingira mazuri kwa klabu zetu kuwatupia macho baadaye.

Hatukatai wala kukataza klabu kusajili wachezaji kutoka nje ya nchi, lakini ifike wakati zianze kufikiria kuwa na timu za vijana kwa wanawake kwa faida yao na nchi kwa ujumla.

Soka la wanawake kwa sasa linakuwa kwa kasi, na imeonekana kuwa soko lao ni rahisi zaidi kuuzika kuliko wanaume.

Klabu ikiweza kutengeneza wachezaji wa kike vizuri, haihitajiki mpaka apitie timu kubwa ili auzike nje ya nchi, ni kiasi cha kuonekana ana uwezo mzuri tu, kucheza Ulaya wala si kazi kubwa kama ilivyo kwa wanaume.


Tumeona wachezaji kama Aisha Masaka, Opah Clement, ambao walicheza nchini, hawakuchukua muda kucheza soka la kulipwa Ulaya, hivyo ni wakati wa klabu nchini kujipambanua na kuwekeza pia katika soka la wanawake.

Tunavikumbusha hata vituo vya akademi kuwa biashara kubwa ya kutengeneza wachezaji na kuwauza haraka nje ya nchi kwa sasa ipo kwa soka la wanawake.

Klabu za Ligi Kuu, zikiwamo za Simba na Yanga, zinatakiwa kuwekeza pia kwa nguvu kwenye soka la wanawake kwa kuwa na timu za chini ya miaka 17 na 20, kwani hawatochukua muda mrefu kabla ya kupata faida.

Tunatambua kupata wachezaji wa kike wa umri huo pia ni kazi, lakini pakiwapo na dhamira ya kweli hilo linawezekana na faida kubwa itaonekana mapema, badala ya kusubiri vipaji kuanza kuonekana vyenyewe.

Sisi tunataka kuona mashindano yajayo ya GIFT tunapeleka timu za U-17 ambazo zitakuwa zimeshindana ndani na kupata nafasi hiyo badala kuzitegemea tu JKT Queens na TDS ambazo zina timu za wanawake za vijana.





Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com


## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

# Klabu zikamilishe usajili mapema kuepuka msongamano mwishoni

**DIRISHA** dogo la usajili kwa timu za Ligi Kuu Tanzania Bara, Ligi ya Championship, First League, na Ligi ya Soka la Wanawake, linatarajiwa kufungwa Jumatano wiki hii.

Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF), limekumbusha kuwa hakutakuwa na muda wa ziada kwa ajili ya usajili. Januari 15 saa 5:59, ndiyo utakuwa mwisho wa kutuma majina kwenye mfumo wa TMS na baada ya hapo hakuna timu yoyote itakayoruhusiwa kufanya hivyo.

Kwa maana hiyo timu inaweza kuwa na mchezaji, imeingia naye mkataba, lakini ikashidwa kumtumia kama itakuwa haijamwingiza kwenye mfumo kwa wakati uliowekwa.

Nimeona timu nyingi ziko kwenye pilikapilika za kusaka wachezaji ambao wanaona watawafaa katika kuboresha vikosi vyao kuelekea mzunguko wa pili wa Ligi Kuu.

Pia nimeona taarifa, tambo na shamra shamra ya kusajili wachezaji wapya, lakini hili liendane na kuwahi kuwaidhinisha.

Imekuwa ni kama kawaida au mazoea, klabu za soka hapa nchini kukimbizana dakika za mwisho kuingiza wachezaji kwenye TMS, dakika chache kabla ya kufungwa.

Ndiyo muda ambao viongozi wa klabu wanakuwa wamejazana kwenye korido za TFF, kufanya kila linalowezekana ili mradi siku hiyo majina yote ya wachezaji yatumwe.

Nadhani ifike wakati klabu ziondokane na tabia hii, badala yake ikifika Januari 15 kuwe na utulivu, huku klabu chache tu ndiyo zibaki kumalizia, badala ya kuwa na hekaheka kwenye mtandao wa TMS kiasi kwamba mfumo unazidiwa.

**Madhara ya mfumo kuzidiwa inajulikana. Ni kwamba majina yaliyotumwa hayaingii katika muda uliokuwa unatakiwa, hivyo baadaye kunatakiwa kuwa na uhakiki wa hali ya juu kujua kama yalitumwa kwa muda sahihi au la. Hapo sasa mchezaji hawezi kucheza mpaka uhakiki ufanyike.**

Madhara ya mfumo kuzidiwa inajulikana. Ni kwamba majina yaliyotumwa hayaingii katika muda uliokuwa unatakiwa, hivyo baadaye kunatakiwa kuwa na uhakiki wa hali ya juu kujua kama yalitumwa kwa muda sahihi au la. Hapo sasa mchezaji hawezi kucheza mpaka uhakiki ufanyike.

Kinachoonekana ni usumbufu mkubwa kwa viongozi wa klabu kuanza kutuma majina siku ya mwisho ya usajili kwani kuna matatizo mengi yanaweza kujitokeza na kuzima usajili wote.

Majina yatakapotumwa mapema hata kama kuna makosa yanayojitokeza kunakuwa na muda wa kuyatatua kabla ya kuyamaliza, tofauti na yakitumwa wakati wa mwisho.

Mbali na mlolongo wa majina mengi kutumwa siku ya mwisho kiasi mpaka mfumo unalemewa, pia tumekuwa tukiona hata baadhi ya timu zikiweka pingamizi kwa wachezaji hao.

Badala yake TFF inaamua klabu kwenda kumalizana. Inaweza kuchukua wiki moja, mbili mpaka mwezi kufanya hivyo. Ni kipindi ambacho mchezaji inabidi akae bila kucheza, hivyo pia ni hasara ya klabu ambayo imesajili mchezaji aliyetakiwa kuisaidia timu.

Haya yote yanaweza kuepukika kama majina yakitumwa mapema. Kwa maana hiyo nazishauri klabu za soka nchini kuwa huu ndiyo muda wa kutuma majina kabla ya kesho kutwa, ili kuepuka hiki ambacho nimekibainisha hapa. Mtakuja kunishukuru baadaye.

TANGAZO

# Mafanikio na mikakati ya Mamlaka ya Mapato ya Zanzibar (ZRA) kuelekea Maadhimisho ya Miaka 61 ya Mapinduzi Visiwani Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu**



*Said Ali Mohammed, Kaimu Kamishna Mkuu ZRA.*

Mamlaka ya Mapato ya Zanzibar (ZRA) imepiga hatua kubwa katika ukusanyaji wa mapato na kuimarisha uchumi wa Zanzibar tangu Mapinduzi ya 1964, kupitia juhudi mbalimbali zinazolenga kuboresha mifumo ya kodi, kuongeza uwazi, na kupanua wigo wa mapato. Mafanikio haya yamechangia maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya Visiwa vya Zanzibar.

Katika kusherehekea miaka 61 ya Mapinduzi mwaka 1964, ZRA ina mafanikio mengi ya kujivunia. Kaimu Kamishna Mkuu wa ZRA Said Ali Mohamed anaelezea kuwa moja ya mafanikio ni kuongezeka kwa mapato ya ndani kupitia juhudi za kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa kodi hasa matumizi ya teknolojia za kisasa kama mifumo ya kielektroniki ya ulipaji kodi, Mamlaka imeweza kupunguza mianya ya upotevu wa mapato na kuhakikisha ulipaji kodi unafanyika kwa uwazi na ufanisi.

Kamishna Said aliezea kuwa ZRA imefanikiwa katika matumizi ya teknolojia ya kisasa kwa kuanzisha mifumo ya kielektroniki, kama vile Virtual Electronic Fiscal Management System (VFMS) na mifumo ya malipo ya kodi kupitia simu za mkononi na benki kitu ambacho kimewarahisisishia walipakodi kufanya malipo kwa haraka na kwa usalama zaidi na kufikia malengo zaidi.

Kutokana na mashirikiano makubwa yanayooneshwa na wadau na walipakodi, ZRA imeweza kufikia na kuvuka lengo la makusanyo lililowekwa katika kipindi cha Julai hadi Disemba 2024 .

Akifafanua taarifa ya makusanyo ya kodi kwa muda wa miezi sita ya kwanza ya Julai hadi Disemba 2024 katika mwaka wa fedha 2024 hadi 2025, Kamishna Said alisema kuwa katika mwezi wa Disemba 2024, ZRA ilikadiriwa kukusanya Tshs. 75.501 bilioni, na ilifanikiwa kukusanya jumla ya Tshs. 75.582 bilioni, ambao ni kutokana na ufanisi asilimia 100.11 ya kiasi kilichokadiriwa kukusanywa. Aidha, alifafanua kuwa makusanyo kwa mwezi wa Disemba ya mwaka wa 2023 yalikuwa ni Tshs. 63.513 bilioni, ambayo yakilinganishwa na makusanyo ya mwezi wa Disemba ya Mwaka 2024 yanaonesha ongezeko la Makusanyo ya Tshs.12.069 bilioni sawa na ukuaji wa makusanyo ya asilimia 19.

"Ufikiaji wa lengo la Makusanyo ya kodi kwa asilimia 102.34 pamoja na mambo mengine umechangiwa na uwekezaji mkubwa katika ujenzi wa miundombinu na huduma za kijamii pamoja na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi Zanzibar unaotokana na utekelezaji wa sera nzuri za kiuchumi za Serikali ya Awamu ya Nane (8) inayoongozwa na Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi," alisema Kamishna Said.

Alisema sababu nyingine ni kuimarika na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi kati ya Zanzibar na Tanzania Bara, zinazotokana na sera na uongozi mzuri wa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, zilizoimarisha mazingira ya ufanyaji wa biashara pande zote mbili za Muungano, sambamba na kuvutia uwekezaji nchini.

Alitaja pia kuimarika kwa mahusiano na ushirikiano kati ya ZRA na wafanyabiashara pamoja na wadau wengine wa Zanzibar na nje ya Zanzibar kulikopelekea kuongezeka kwa ulipaji kodi wa hiari kama sabbau mojawapo ya kuongezeka kwa makusanyo visiwani humo. .

"Si hayo tu bali pia sababu zingine za kuongezeka kwa makusanyo ni kuimarika kwa uzuwiaji wa Kodi (Withholding Tax) kunakofanywa na Mawakala wa uzuwiaji hali inayotokana na utekelezwaji wa Sera na Miradi mbalimbali ya kimaendeleo chini ya Serikali ya Awamu ya Nane (8) inayoongozwa na Hh. Dkt Hussein Ali Mwinyi, kuimarika kwa miundombinu ya Bandari hususan Bandari ya Mkoani Pemba ambayo inapelekea kuimarika kwa shughuli za kiuchumi," alifafanua Kamishna Said.

Kamishna Said alisema kuwa ZRA inawashukuru walipakodi wote kwa kuwajibika kwa hiyari katika kipindi hicho inawasisitiza kuendelea kuwajibika kwa mujibu wa Sheria ili waweze kutimiza wajibu wao wa Kisheria katika Kulipa Kodi. Kamishna Said alieleza kuwa pia ZRA imepiga hatua kuwa katika kufanya kampeni za uhamasishaji na elimu ya Kodi ambapo mamlaka imeendesha kampeni mbalimbali za elimu kwa walipakodi ili kuwaelimisha kuhusu umuhimu wa kulipa kodi kwa maendeleo ya nchi ambapo imeongeza uelewa wa wananchi kuhusu wajibu wao wa kulipa kodi na kupunguza changamoto za ukwepaji kodi.

Akielezea mikakati ya ukusanyaji wa kodi kwa kipindi Januari hadi juni mwaka jana, Kamishna Said alisema kuwa kwa madhumuni ya kuendelea na hatua za ukusanyaji katika nusu ya pili ya Januari – Juni 2025 ya mwaka wa fedha mwaka 2024 hadi 2025, ZRA itaendelea kutekeleza mikakati yake kama kuendelea kutoa elimu ELIMU YA KODI kwa makundi mbali mbali ya walipakodi na wananchi ili kutoa uelewa wa masuala mbali mbali ya kodi ikiwemo matumizi sahihi ya Mifumo ya Kodi.

Aidha Kamishna Said aliongeza kuwa pia ZRA inaendeleza mkakati wake wa kuimarisha vitengo vya Ukaguzi kwa lengo la kuzuia ukwepaji wa kodi unaoweza kufanywa na wafanyabiashara wasio waaminifu wenye lengo la kujinufaisha binafsi kwa kuikosesha Serikali mapato yake sambamba na kubaini mwenendo wa utii wa Sheria za Kodi kwa Wafanyabiashara hao.

"Pia mkakati wetu mwingine ni kuendelea kufanya ziara na matukio mbali mbali ya kielimu kwa walipakodi ili kutambua na kutatua changamoto za wafanyabiashara na migogoro ya Kikodi kwa wakati ambapo matukio haya yanatarajiwa kuongeza uwajibikaji wa hiyari katika kulipa Kodi, " alifafanua Kamishna Said.

Alielezea zaidi kuwa ZRA itaendelea kuwa kuwa karibu na Wafanyabiashara kwa kuwasiidia katika kurahisisha mazingira ya biashara kisheria (Trade Facilitation) kwa kutoa msaada wa karibu kwa Wafanyabiashara na kuwajengea mazingira ya kustawisha biashara zao hususan kwa Walipakodi Wapya.

Aliongeza kuwa ZRA itaendesha zoezi la kuweka Kambi maalum za Walipakodi (Tax Clinics) katika maeneo mbali mbali zenye lengo la kutoa huduma za Kodi kwa Karibu ambapo mkakati huu utaweza kuongeza wigo wa kusajili wafanyabiashara mbalimbali wanaofanya biashara zao Zanzibar kwa kusogeza huduma ya usajili maeneo yao.

Alisema kuwa ZRA itaendeleza weledi kwa watumishi wake kwa kuwapatia mafunzo stahiki, usimamizi makini, na huduma bora kwa walipakodi (Customer Services) sambamba na kusimamia maadili ya wafanyakazi .

" Miongoni mwa mafanikio ZRA tunajivunia tukiwa tunaelekea kusherekea Mapinduzi ya 61 visiwani mwetu ni kuboresha huduma kwa wateja ambapo tumeweza kuanzisha vituo vya huduma kwa wateja, kuongeza usaidizi kwa walipakodi, na kuweka mifumo rahisi ya malipo. Hii imeongeza imani ya walipakodi na kurahisisha utendaji wa mamlaka," aliongeza Kamishna Said.

ZRA pia inajivunia ushirikiano wa karibu na mamlaka nyingine za mapato ndani ya Tanzania na nchi jirani, pamoja na mashirika ya kimataifa, ili kubadilishana uzoefu, teknolojia, na mbinu bora za ukusanyaji wa kodi.

Kamishna Said alisema kuwa ZRA imekuwa chachu ya mchangiaji wa maendeleo ya kiuchumi visiwani humo kwani mapato yanayokusanywa yamechangia miradi muhimu ya maendeleo, kama vile ujenzi wa miundombinu, huduma za afya, elimu, na miradi ya maji safi. Hii inaonyesha mchango mkubwa wa mamlaka katika kuboresha maisha ya wananchi wa visiwa vya Zanzibar.

Mafanikio ya ZRA yanatokana na juhudi za pamoja za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), wafanyakazi wa mamlaka , na wananchi wa Zanzibar. Kwa kusimamia kwa ufanisi ukusanyaji wa mapato, ZRA imekuwa kiungo muhimu katika kuhakikisha maendeleo endelevu ya Zanzibar. Hata hivyo, bado kuna nafasi ya kuimarisha zaidi juhudi hizi ili kuhakikisha kuwa mapato yanakusanywa kwa uwazi, usawa, na ufanisi," alielezea Kamishna Said .

ZANZIBAR REVENUE AUTHORITY

MAMLAKA YA MAPATO ZANZIBAR

MIAKA 61 YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR
1964 2025

Miaka 61
YA MAPINDUZI
YA ZANZIBAR

1964 - 2025

IKIWA NI KATIKA KUADHIMISHA MIAKA 61 YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR UONGOZI PAMOJA NA WAFANYAKAZI WOTE WA MAMLAKA YA MAPATO ZANZIBAR (ZRA), WANAUNGANA NA WANANCHI WOTE WA ZANZIBAR NA WATANZANIA KWA UJUMLA KUMPONGEZA MHE. RAIS WETU, DKT. HUSSEIN ALI MWINYI PAMOJA NA KUMUOMBEA KHERI NA FANAKA KATIKAKUIONGOZA ZANZIBAR NA KUILETEA MAENDELEO.



Mh. Dr.Hussein Mwinyi, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, (kulia) akiongoza wananchi kufanya usafi kwenye maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam kabla ya ujio wa marais wa Afrika kwenye mkutano wa nishati unaotarajiwa kufanyika hivi karibuni. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Kaya 250 zagoma kuwapeleka watoto shuleni

**Na Mwandishi Wetu,** MKURANGA

KAYA 250 zimegoma kuwaandikisha watoto wao darasa la awali na msingi mwezi huu baada ya kuibuka mgogoro wa mipaka ya ardhi kati ya vijiji vitatu vya Chamgoi, Kisegese na Vianzi wilayani Mkuranga, mkoa wa Pwani.

Mgogoro huo umeibuka baada ya wanakijiji wa Kisegese kupinga eneo lao lenye ukubwa wa hekta 1,246.6 kuchukuliwa bila maridhiano na kijiji jirani cha Chamgoi. Inadaiwa kuna kusudio la kulifanya eneo hilo kuwa hifadhi ya msitu.

Kutokana na kuwapo mgogoro huo, wazazi wa Kisegese wamegoma kuandikisha watoto wao shuleni katika Kituo Shikizi cha Vinyaga wilayani humo.

Akizungumza katika mkusanyiko wa wanakijiji wa Kisegese wiki iliyopita, mmoja wa walimu wa shule hiyo, Hossein Kikumbo, alisema mgogoro huo umeathiri elimu ya awali na msingi kwa kuwa mwaka huu hajaandikisha mtoto hata mmoja kuingia shuleni huko kutokana na mgogoro huo wa mpaka.

Mwalimu Kikumbo alisema kituo hicho cha shule ambacho hivi sasa kina wanafunzi 132, mwaka huu hawajajiandikisha wanafunzi wapya kutokana na wazazi kuweka mgomo, wakipinga viongozi wa tarafa ya Mkamba na kata ya Kisegese kudaiwa kushirikiana na kijiji cha Chamgoi kuweka mipaka katika eneo la kijiji chao cha Kisegese.

Mmoja wa wakazi wa Kisegese, Rukia Msumi (80), alidai wamechoshwa na alichokiita "kunyanyaswa na viongozi wa tarafa na kata ambao wanataka kumega ardhi yao ili ichukuliwe na kijiji jirani kwa lengo la kuweka hifadhi ya mali asili".

Rukia alidai anaumia kuona viongozi wao wanataka kuwadhulumu ardhi ili isomeke ya kijiji cha Chamgoi wakati si kweli kwa kuwa mipaka iliyopo inaonesha eneo hilo liko Kisegese.

Alimwomba Rais Samia Suluhu Hassan na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa kuingilia kati kutatua mgogoro huo uliosababisha wazazi kususia kuwapeleka watoto wao kuandikishwa shuleni mwaka huu.

**Mmoja wa wakazi wa Kisegese, Rukia Msumi (80), alidai wamechoshwa na alichokiita "kunyanyaswa na viongozi wa tarafa na kata ambao wanataka kumega ardhi yao ili ichukuliwe na kijiji jirani...**

Rukia alisema mgogoro huo ulioanza mwaka 2022, umekuwa na athari kubwa kwa jamii, baadhi ya wanakijiji wakishindwa kujihusisha na kilimo na shughuli zinginezo kutokana na wasiwasi uliopo wa kuondolewa katika eneo hilo.

Mkazi mwingine wa kijiji hicho, Amanuel Hosea (65) alidai kumekuwa na sintofahamu ya viongozi wa tarafa na kata kulazimisha kuweka mipaka katika kijiji kingine. Licha ya malalamiko yao kufikishwa ngazi ya wilaya, hawajasikilizwa.

Hosea alidai mawe ya mipaka iliyowekwa kwenye kijiji cha Chamgoi na viongozi wa tarafa na kata si sahihi kwa kuwa wanajua hekta 1,246.6 ziko katika kijiji cha Kisegese.

Jiroti Masanja (56), mkazi mwingine wa kijiji hicho, alidai kuwa awali aliyekuwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mkuranga, Mshamu Munde aliagiza vijiji hivyo vitatu vikae pamoja kujadili mgogoro huo, lakini anashangaa kuona viongozi wanaweka mipaka pasina kushirikisha wananchi.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kisegese, Theonas Paulo, alipotafutwa na mwandishi wa habari hii kuzungumzia mgogoro huo, alikiri kuwapo kwake, akidokeza kuwapo jitihada za viongozi kusaka suluhu, lakini imeshindikana.

Paulo alisema kuwa kwa hatua iliyopo sasa, kuna haja ngazi za juu za uongozi serikalini kuingilia kati kutatua mgogoro huo kwa kuwa unaathiri maendeleo.

Paulo alisema mgogoro huo umesababaisha watu kuishi kwa wasiwasi, baadhi wanashindwa kufanya kazi za maendeleo kutokana na hofu ya kuondolewa katika kijiji hicho.

"Tunamwomba Rais Samia, Waziri Mkuu Majaliwa, Mbunge wetu (Abdallah) Ulega kuingilia kati mgogoro huu haraka ili kuokoa maisha ya wanakisegese," alisema.

Akizungumzia mgogoro huo, Mwenyekiti wa Kitongoji cha Nyandege, kijijini Kisegese, Tatu Mohammed, alisema robo tatu ya Kisegese imeingia katika mgogoro na kijiji jirani.

Tatu alisema wanakijiji cha Kisegese wako tayari kukaa pamoja na wenzao kwa ajili ya mazungumzo ya kusaka suluhisho la mipaka ya vijiji hivyo vitatu vya Chamgoi, Kisegese na Vianzi.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***


## TANGAZO LA MNADA

Dar state, Dc classic, Workethic, Crisam and Marmboto auctioneer Company Kwa idhini tuliyopewa na **FANIKIWA MICROFINANCE COMPANY** tunapenda kuutarifu umma kuwa Tutafanya Mnada Wa nyumba na magari Jijini Dar es saalam, na Arusha Mteja anashauriwa kulipa deni ndani ya siku 14 za hili Tangazo vinginevyo Mnada utaendelea kama Tarehe ya Mnada inavyoonekana hapa chini.

| | Client name | Type of the Collateral | Location of collateral | Auctioneer | Date |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Bakari Seif Bakari | Nissan X trail T696BUC | Dar es salaam | Dar state | 28.01.2025 |
| 2 | OTHUMANI JUMA MAUMBA | BMW X5 T229DHV | Dar es salaam | Dc classic | 28.01.2025 |
| 3 | Laban Joseph Nkembo | Landrover Rangerover T686DJN | Dar es salaam | DC Classic | 28.01.2025 |
| 4 | YUSUPH VAIS LUVANGA | Mitsubishi Pajeromini-T743DTN | Dar es salaam | workethic | 28.01.2025 |
| 5 | Andrew Vicent Rwechungura | Toyota Mark 11 T199DFP | Dar es salaam | Crisam | 28.01.2025 |
| 6 | Faraji Michael Juma | Plot of land Located at Sekei Arusha | Arusha | Marmboto | 28.01.2025 |
| 7 | Beatrice George Mollel | Plot of land located at Mlimani Arusha | Arusha | Marmboto | 28.01.2025 |

**Masharti ya Mnada.**

1. Mnunuzi atakeyeshinda atalipa 25% (au Zaidi) ya bei iliyofikwa kwenye mnada na salio la (75%) litalipwa ndani ya siku kumi nne(14) kuanzia tarehe ya mnada.
2. Endapo mnunuzi atashindwa kulipa salio kwa mda uliotolewa atakuwa amepoteza haki zote na mali itauzwa upya.
3. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe ya Tangazo.

**Kwa Mawasiliano Piga 0677014355(Fanikiwa)**


# Bil 329/- kutumika miradi ya barabara na madaraja

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

ZAIDI ya Sh. bilioni 329.56 zinatarajiwa kutumika kwa ajili ya utekelezaji miradi ya ujenzi wa barabara zenye urefu wa Km 189.6 mkoani Morogoro.

Meneja wa Wakala wa Barabara (TANROADS ) Mkoa wa Morogoro, Alinanuswe Kyamba alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa kikao cha 42 cha Bodi ya Barabara mkoani Morogoro.

Alitaja barabara zitakazojengwa ni pamoja na Ubena Zomozi-Ngerengere-Kizuka Army Camp ya Km 11.6, Ifakara-Mbingu Km 62.5, Mbingu-Chita Km 37.5, Bigwa-Mvuha Km 78.

Kyamba alisema jitihada mbalimbali zimefanywa na serikali katika mwaka unaomalizika kwa kutengeneza na kukarabati miundombinu ya barabara na madaraja yakiwamo yalioathiriwa na mvua ya El-nino na Kimbunga Hidaya na kurudisha mawasiliano kama kawaida.

"Kiasi cha Sh. bilioni 4.7 kimetumika kwa ajili ya kurejesha mawasiliano katika barabara na madaraja yaliyoathiriwa na mvua za El-nino na Kimbunga Hidaya.

"Serikali pia imetenga Sh. bilioni 37.8 kupitia ufadhili wa Benki ya Dunia ili kujenga madaraja maeneo ya Chakwale na Nguyami katika wilaya ya Gairo," alisema meneja huyo.

Kyamba alitaja madaraja mengine kuwa ni Mjonga, Bwage na Doma yaliyoko wilaya ya Mvomero pamoja na Ngerengere na Kihonda katika wilaya ya Morogoro ambapo Sh. bilioni 16.153 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa maradaja ya Namhanga na Fuluwa na kufanya jumla ya Sh. bilioni 53.994 kutumika kwa kazi hizo. Awali Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima alielekeza Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) kushirikisha mabaraza ya madiwani kutekeleza miradi yao ili kuwa na uelewa wa pamoja katika kazi hizo kwa kuwa hao ndiyo wenye maeneo.

Pia alielekeza Jeshi la Polisi kuweka kamera maalumu barabara kuu hasa kwenye maeneo korofi yanayokumbwa na ajali ili kuwadhibiti madereva wazembe na wasiofuata sheria, kanuni na taratibu za usalama barabarani.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, SACP Alex Mkama alisema changamoto kubwa ni baadhi ya maeneo kukosa mawasiliano, hivyo kushauri serikali na wadau wengine wa mawasiliano kuona uwezekano wa kuweka mawasiliano barabara kuu hasa katika eneo la Iyovi wilayani Kilosa ambako kumekuwa na changamoto za ajali ili jeshi hilo liwafuatilie kwa urahisi madereva kupitia mfumo wao.

Changamoto nyingine iliyotajwa ni kwa madereva wa serikali kutokuwa makini barabarani na kusababisha ajali kutokana na uzembe na kutofuata sheria za usalama barabarani.

TANGAZO

MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

# TAARIFA KWA UMMA

## Mwaliko Wa Mafunzo ya Matumizi ya Mfumo Mpya wa Usimamizi wa Kodi za Ndani (IDRAS) – Usajili wa Vyombo Vya Moto na Utoaji wa Leseni za Udereva

***Dar es Salaam, 06 Januari, 2025***

Katika jitihada za kuboresha huduma kwa mlipakodi na umma kwa ujumla, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ipo katika mchakato wa kujenga mfumo wa kisasa wa usimamizi wa kodi za ndani uitwao (IDRAS). Mfumo wa kisasa wa kielektroniki utakaoanza kutumika hapa nchini kwa awamu. Awamu ya kwanza itazinduliwa rasmi na kuanza kutumika katika mwezi **Januari 2025,** ikiwa na moduli zinazohusisha:

1) Usajili na usimamizi wa vyombo vya moto (magari, pikipiki, tela, n.k)
2) Utoaji wa Leseni za Udereva

Ikiwa ni maandalizi ya utumiaji wa mfumo huo mpya, TRA imeandaa mafunzo juu ya mfumo huo kwa lengo la kuwajulisha watumiaji juu ya maboresho yaliyofanyika na kuwawezesha kutumia mfumo huu bila changamoto yoyote. Mafunzo hayo yataendeshwa kwa njia ya masafa **(virtual training)** ili kuwezesha ushiriki wa watu wengi kwa pamoja. Mambo muhimu yatakayofundishwa ni pamoja na:

i). Utangulizi juu ya sifa za mfumo mpya
ii). Mambo muhimu ya kuzingatia ili kuweza kutumia mfumo mpya
iii). Maombi ya leseni ya Udereva (Leseni ya mafunzo ya udereva (Provisional/Learner driving license), Leseni mpya, kuhuisha leseni, pamoja na maombi ya nakala ya leseni)
iv). Usajili wa shule za mafunzo ya udereva
v). Usajili na usimamizi wa vyombo vya moto (usajili mpya, kubadili umiliki, kubadili taarifa, kubadili mmiliki mwenza, kufuta usajili, kurudia usajili, kufunga/kufungua chombo, kusitisha kwa muda matumizi ya chombo cha biashara, Kurekebisha taarifa za chombo baada ya usajili)
vi). Usajili wa wauzaji wa vyombo vya moto (car dealers)
vii). Usajili wa watengenezaji wa ndani wa vyombo vya moto (local manufacturers)

**Ratiba ya mafunzo ni kama ifuatavyo:**

| Tarehe ya Mafunzo | Namna ya mafunzo | Namna ya Kushiriki Mafunzo | Muda wa Kuanza Mafunzo |
|---|---|---|---|
| 9 Januari 2025 | Njia ya masafa ***(Virtual Training)*** | 1. Pata link/anuani kwa kutembelea ***Tovuti* (*www.tra.go.tz*)** au akaunti zetu za mitandao ya kijamii (***Instagram:****tratanzania*, ***Facebook:****tratanzania*, ***Twitter:****tratanzania*)<br>2. Shiriki kupitia youtube **@traonlinetv** | Saa 10:00 Jioni |
| 10 Januari 2025 | Njia ya masafa ***(Virtual Training)*** | 1. Pata link/anuani kwa kutembelea ***Tovuti* (*www.tra.go.tz*)** au akaunti zetu za mitandao ya kijamii (***Instagram:****tratanzania*, ***Facebook:****tratanzania*, ***Twitter:****tratanzania*)<br>2. Shiriki kupitia youtube **@traonlinetv** | Saa 10:00 Jioni |
| 11 Januari 2025 | Njia ya masafa ***(Virtual Training)*** | 1. Pata link/anuani kwa kutembelea ***Tovuti* (*www.tra.go.tz*)** au akaunti zetu za mitandao ya kijamii (***Instagram:****tratanzania*, ***Facebook:****tratanzania*, ***Twitter:****tratanzania*)<br>2. Shiriki kupitia youtube **@traonlinetv** | Saa 4:00 Asubuhi |

Ikumbukwe kuwa pamoja na mafunzo haya, TRA pia itatoa mafunzo zaidi na kwa makundi mahsusi kwa njia mbalimbali ikiwemo semina, vipindi vya redio na televisheni, vipeperushi na kutoa miongozo ya utumiaji (User Guides). Taarifa juu ya mafunzo zitaendelea kutolewa kwa njia mbalimbali ili kuhakikisha kuwa walipakodi na umma kwa ujumla wanapata elimu ya kutosha kuhusu matumizi ya mfumo wa IDRAS.

Kwa taarifa zaidi, tembelea ofisi za TRA zilizo karibu nawe au wasiliana nasi kupitia:

**Tovuti** : **www.tra.go.tz**
**Namba za Simu Bila Malipo** : **0800 750 075 au 0800 780 078**
**WhatsApp** : **0744 23 33 33**
**Barua pepe** : **huduma@tra.go.tz au services@tra.go.tz**

**"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"**
**Imetolewa na:**

**IDARA YA HUDUMA NA ELIMU KWA MLIPAKODI**

# MATANGAZO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

## TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya Kifungu cha 19 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania)**

**TAARIFA** inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea maombi ya Leseni ya Muda ya Kuzalisha Umeme kutoka kwa kampuni ya Tanzania Tooku Garments Company Ltd. EWURA inakaribisha maoni au pingamizi dhidi ya maombi hayo. Taarifa za mwombaji, mitambo na aina ya leseni iliyoombwa zimetolewa hapa chini:-

| KIFUNGU | MAELEZO |
|---|---|
| **Jina na anuani ya Mwombaji** | Tanzania Tooku Garments Company Limited, S.L.P 12112, Ubungo, Dar es salaam. |
| **Mahali ulipo Mtambo** | Kiwanja Na. 22 & 23, Makuburi, Ubungo. Dar es salaam. |
| **Taarifa za Wanahisa** | Ji Yao, P O Box 12112, Dar es Salaam, **100%** |
| **Maelezo ya Mtambo** | Mtambo wa kuzalisha umeme wa Megawati (MW) Tatu (3 MW) kutumia nishati ya jua. Umeme utakaozalishwa utakua kwa matumizi binafsi. |
| **Aina na Muda wa Leseni** | Leseni ya Muda Kuzalisha Umeme kwa matumizi binafsi kwa muda wa miaka mitano (5) |

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi kuhusu maombi haya awasilishe kwa maandishi ndani ya siku ishirini na moja (21) tangu siku ya kutolewa kwa tangazo hili. Nyaraka za maombi ya leseni zinaweza kuoneshwa kwa mtu atakayewasilisha maombi kwa maandishi.

Imetolewa na:-
**Mkurugenzi Mkuu**
**06 Januari 2025**

Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA , 41104 Tambukareli, S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania
Simu: +255 26 2329002 – 4 • Nukushi: +255 26 2329005 • Barua Pepe: info@ewura.go tz

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

## TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya Kifungu Na. 126 cha Sheria ya Petroli, Sura ya 392 na Kanuni Na. 4(1&2(b)) ya Kanuni za Mafuta (Gesi Asilia) (Shughuli za Usafirishaji na Usambazaji) ya Mwaka 2018**

**TAARIFA**inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea maombi ya Kampuni ya **Pan African Energy Tanzania Limited** kwa ajili ya kibali cha ujenzi wa bomba la kusambaza gesi asilia yenye urefu wa mita 870 kutoka bomba la usambazaji wa gesi asili lililopo barabara ya Nyerere hadi kituo cha gesi asilia cha Victoria Services kilichopo eneo la viwanda Kipawa, kiwanja namba 112, kandokando ya barabara ya Nyerere, Manispaa ya Ilala, Mkoa wa Dar Es Salaam.

Hivyo, Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi dhidi ya ombi tajwa hapo juu, afanye hivyo kwa maandishi na kuwasilisha EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku kumi na nne toka tarehe ya tangazo hili.

**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**
**Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA, 41104 Tambukareli**
**S. L. P 2857, Dodoma.**

**Simu: +255-26 2329003-3; Nukushi: +255-26 2329005;**
**Namba ya Bure 0800110030;**
**Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: http.//www.ewura.go.tz**

**Imetolea na:**
**Mkurugenzi Mkuu**
**EWURA**

Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA , 41104 Tambukareli, S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania
Simu: +255 26 2329002 – 4 • Nukushi: +255 26 2329005 • Barua Pepe: info@ewura.go tz

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

## TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya kifungu Na 126 cha Sheria ya Petroli ya mwaka 2015 na Kanuni Na. 6(1) ya Kanuni za Mafuta (The Petroleum (Natural Gas) (Transmission and Distribution Activities) Rules, GN No. 176 of 2018).**

**TAARIFA** inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea maombi ya **Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC)** kwa ajili ya kibali cha ujenzi wa njia ya kusambaza gesi asilia yenye urefu wa mita 155 kutoka bomba la usambazaji wa gesi asilia la Ubungo - Mikocheni. Bomba linalotarajiwa kujengwa litakatiza Barabara ya Sam Nujoma ili kuunganisha kituo cha kushindilia gesi asilia cha TAQA Dalbit Tanzania Limited kilichopo Manispaa ya Ubungo, Mkoa wa Dar Es Salaam.

Hivyo, Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi dhidi ya ombi tajwa hapo juu, afanye hivyo kwa maandishi na kuwasilisha EWURA kwa anwani iliyotajwa hapa chini ndani ya siku kumi na nne toka tarehe ya tangazo hili.

**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**
**Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA, 41104 Tambukareli**
**S. L. P 2857, Dodoma.**

**Simu: +255-26 2329003-3; Nukushi: +255-26 2329005;**
**Namba ya Bure 0800110030;**
**Barua pepe: info@ewura.go.tz Tovuti: http.//www.ewura.go.tz**

**Imetolea na:**
**Mkurugenzi Mkuu**
**EWURA**

Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA , 41104 Tambukareli, S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania
Simu: +255 26 2329002 – 4 • Nukushi: +255 26 2329005 • Barua Pepe: info@ewura.go tz

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)

## TAARIFA KWA UMMA

**(Imetolewa chini ya Kifungu cha 19 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania)**

**TAARIFA** inatolewa kwa umma kwamba Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imepokea maombi ya Leseni ya Muda ya Kuzalisha Umeme kutoka kwa kampuni ya Luponde Hydro Ltd. EWURA inakaribisha maoni au pingamizi dhidi ya maombi hayo. Taarifa za mwombaji, mitambo na aina ya leseni iliyoombwa zimetolewa hapa chini:-

| KIFUNGU | MAELEZO |
|---|---|
| **Jina na anuani ya Mwombaji** | Luponde Hydro Ltd, S.L.P. 555, Mufindi, Iringa. |
| **Mahali ulipo Mtambo** | Kiwanja Na. 43868 – MBYLR, Uliwa, Njombe Mjini |
| **Taarifa za Wanahisa** | 1. Rift Valley Energy Tanzania Ltd, S.L.P. 555, Mafinga, Iringa, **99.9%**<br>2. Meridiam Africa Investments 2<br>4 Place de L'Opera, 75002, Paris, Ufaransa, **0.1%** |
| **Maelezo ya Mtambo** | Mtambo utakao tumika kuzalisha umeme kiasi cha Megawati (MW) mbili (2 MW), Maji ndio chanzo cha cha Uzalishaji. |
| **Aina na Muda wa Leseni** | Leseni ya Muda kwa ajili ya kuzalisha umeme kwa miaka Mitatu (3) |

Mtu yeyote mwenye maoni au pingamizi kuhusu maombi haya awasilishe kwa maandishi ndani ya siku ishirini na moja (21) tangu siku ya kutolewa kwa tangazo hili. Nyaraka za maombi ya leseni zinaweza kuoneshwa kwa mtu atakayewasilisha maombi kwa maandishi.

Imetolewa na:-
**Mkurugenzi Mkuu**
**03 Januari 2025**


Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA , 41104 Tambukareli, S.L.P. 2857, Dodoma, Tanzania
Simu: +255 26 2329002 – 4 • Nukushi: +255 26 2329005 • Barua Pepe: info@ewura.go tz

Nipashe
# Spotika



BRENTFORD... UKURASA 14

# MABEKI 5 WA KUZIBA NAFASI YA ALEXANDER-ARNOLD LIVER



KIMMICH

**LIVERPOOL,** England

MSIMU wa 2024/25 unaweza kuwa wa 'kichawi' kwa Liverpool, lakini inaweza kuwa kampeni kubwa ya kubeba mataji kiasi fulani.

Mohamed Salah, Virgil van Dijk na Trent Alexander-Arnold wote mikataba yao inaelekea mwisho. Ingawa mashabiki wanamatumaini nyota hao kubaki hapo Anfield, kuna uwezekano wa kweli kwamba kocha Arne Slot atangia msimu wa 2025/26 bila angalau mmoja wao.

**Mwenye uwezekano mkubwa zaidi wa kuondoka ni Alexander-Arnold. Beki huyo wa pembeni ameonesha wazi kwamba anataka kuondoka katika klabu yake hiyo ya utotoni.**

Real Madrid ndiyo wenye nafasi kubwa zaidi ya kumsajili kutokana na yeye mwenyewe kuonesha nia hiyo.

Makala haya inawaangalia mabeki watano ambao wanaweza kuziba nafasi ya Alexander-Arnold pale Liverpool kama ataondoka mwishoni mwa msimu huu kwa uhamisho wa bure.

**5. Lutsharel Geertruida**

Geertruida alikuwa nahodha wa kocha Slot kule Feyenoord, na kulikuwa na ripoti msimu wa majira ya joto uliopita kwamba bosi huyo mpya wa Liverpool alikuwa na mpango wa kumleta beki huyo wa pembeni wa Uholanzi hapo Anfield.

Hata hivyo, hatua hiyo haikufanyika na badala yake Geertruida alisaini kwenda RB Leipzig.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, ameonesha uchezaji wake wa kuvutia na kocha Marco Rose anamtumia kama beki wa kati huko Leipzig. Kwa Slot, Geertruida kwa ujumla alifanya kazi nzuri chini yake.

**4. Joshua Kimmich**

Kimmich kwa ujumla amechanganyikiwa kwa muda wa miaka kadhaa iliyopita, lakini hoja inaweza kutolewa kwamba kiwango chake bora zaidi katika siku za hivi karibuni kilifika wakati Thomas Tuchel alipomrudisha kama beki wa kulia kwa kipindi cha pili cha msimu wa 2023/24 pale Bayern Munich.

Vincent Kompany amemruhusu Kimmich kucheza katika safu ya kiungo, na Mjerumani huyo ameonesha mara kadhaa muhula huu kwamba anabaki kuwa mwanasoka maalum. Uchezaji wake dhidi ya RB Leipzig kabla ya mapumziko ya msimu wa baridi ulikuwa mzuri sana na ukumbusho wa tishio.

Kimmich anaweza kwa kiasi fulani kufidia kuondoka kwa Trent, lakini ikizingatiwa kwamba kuna uwezekano kutakuwa na klabu kadhaa zinazomuwania mara tu mkataba wake na Bayern Munich utakapomalizika Juni, angechagua kucheza beki wa kulia wa Liverpool? Yeye anataka kucheza beki wa kati.

Slot anaweza kuhitaji kufanya ushawishi kwa sababu Mjerumani huyo anaweza kuwa mbadala mzuri.

**3. Jeremie Frimpong**

Imepita muda tangu Frimpong acheze katika safu ya nne ya nyuma, na kuna uwezekano wa Slot kubadili mbinu kwa ajili ya Mholanzi huyo. Alikuwa bora sana kule Bayer Leverkusen mwaka 2024.

Frimpong alikuwa mmoja wa mabeki tegemeo kwa kocha Xabi Alonso msimu uliopita na amebaki kuwa tegemeo kubwa upande wa kulia msimu huu.

Beki huyo wa pembeni ana nguvu za ajabu na ni mchangiaji wa kutegemewa katika kusukumiza mashambulizi mbele, ingawa anafanya kazi yake kwa njia tofauti kabisa na Alexander-Arnold.

**2. Pedro Porro**

Mashabiki wa Liverpool wanaweza kudharau matarajio ya kumsajili Porro, ambaye amevumilia msimu mgumu wa 2024/25, lakini kiwango kikubwa cha raia huyo wa Hispania kinaweza kuhusishwa na wingi wa dakika ambazo alihitajika kucheza katika kipindi cha miezi 18 iliyopita.

Kuna kufanana kwa staili ya uchezaji kati ya Porro na Alexander-Arnold. Wawili hao ni mafundi bora wenye uwezo wa kufungua ulinzi kupitia safu zao, na bila shaka, kumekuwa hakuna maswali juu ya uwezo wao wa ulinzi.

Hata hivyo, Porro labda amepimwa vibaya kuhusiana na suala hili, wakati Trent amejilinda vema msimu wa 2024/25 - bila kujali uchezaji wao dhidi ya Manchester United.

Uzoefu wa Porro katika Ligi Kuu England ni wa kutosha, na ikiwa Liverpool wana nia ya kumbadilisha beki wao wa kulia na mtu wa wasifu sawa, mchezaji huyo wa Kimataifa wa Hispania anaweza kuwa mchezaji wao.

**1. Conor Bradley**

Baadhi ya mashabiki wa Liverpool wanaweza kuhoji kuwa hakuna haja ya klabu kutumia fedha nyingi kununua beki mpya wakati kiwango ambacho Bradley amefikia ni cha juu zaidi.

Mhitimu huyo wa akademi yao alijaza vizuri nafasi kwa kipindi kifupi msimu uliopita na tayari ameingiza kwenye hatua kubwa zaidi za 'Wekundu' hao.

Bradley ni beki wa pembeni anayefanya vizuri katika awamu zote. Yeye ni mlinzi mkali zaidi kuliko Trent na ni bora anapoingia katika tatu ya mwisho. Bradley ni mkimbiaji zaidi na mchanganyaji na amejidhihirisha ndani ya mfumo wa sasa wa Slot.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, anaonekana kuwa tayari kujaza pengo lolote linalowezekana, na utafutaji wa beki wa kulia wa Liverpool katika msimu wa majira ya joto unaweza usiwe na maana, wakati yeye akiwamo.

## ISIKUPITE

USHINDI wa bao 1-0 ilioupata Pyramids FC ugenini dhidi ya Sagrada Esperanca ya Angola juzi unaifanya kufuzu hatua ya robo fainali ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa mara ya kwanza katika historia ya klabu hiyo tangu ilipoanzishwa mwaka 2008 jijini Cairo, Misri.



Extra Time

# WACHEZAJI SABA WALIOPUNGUZWA BEI



ALPHONSO DAVIES

**LONDON,** England

SOKO la uhamisho wa dirisha la Januari linajulikana kuwa ni gumu. Hata timu zinazoheshimika sana kwa kusajili zinakuwa na wakati mgumu kupata kile wanachokitaka.

Soko hili la la majira ya baridi kwa ujumla hujikita katika hali ya kukatisha tamaa, licha ya klabu kutamani kutatua masuala ambayo yamejitokeza katika nusu ya kwanza ya msimu.

Huku timu zikichukizwa na kupoteza ubora wao katikati ya msimu, hesabu mara nyingi huongezeka sana.

Hata hivyo, bado kuna thamani kubwa ya kuibuliwa wakati wa dirisha la Januari, huku nyota wakiuzwa na wachezaji kuingia miezi sita ya mwisho ya mikataba yao.

Hapa tunawaangalia wachezaji saba ambao bei yao imepunguzwa ili kufanikisha usajili wao Januari hii, hawa hapa...

**1. Jonathan David**
**Klabu zinazomtaka: Arsenal, Man Utd, Tottenham**
**Ada inayowezekana: Pauni milioni 15 hadi 20**

Ni Robert Lewandowski, Harry Kane na Erling Haaland pekee walifunga mabao mengi zaidi ya Jonathan David mwaka 2024. Mchezaji huyo wa Kimataifa wa Canada alicheza mechi 36 kati ya mechi 50 za mwaka mzima wa kalenda - jambo lililovutia sana kutokana na kwamba alikuwa akichezea Lille.

David amezivutia klabu za juu za Ulaya na kumalizika kwa mkataba wake wa sasa msimu huu wa majira ya joto kunamaanisha kuwa yuko tayari kujadili mustakabali wake na klabu nyingine kipindi hiki cha majira ya baridi.

Ingawa kishawishi kitakuwa cha kusubiri hadi mwisho mwa msimu na kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, bila malipo, kumwaga fedha Januari hii kunaweza kuhakikishia saini ya mshambuliaji huyo wa kati.

**2. Alphonso Davies**
**Klabu zinazomtaka: Arsenal, Chelsea, Liverpool, Man City, Man Utd**
**Ada inayowezekana: Pauni milioni 20 hadi 25**

Ukizungumzia wachezaji wa Kimataifa wa Canada ambao mikataba yao inaisha msimu huu wa majira ya joto, Alphonso Davies naye yumo. Wakati Bayern Munich wanatamani sana kumfunga beki huyo wa kushoto kwa mkataba mpya, kuna hisia zinazoongezeka kuwa hii inaweza kuwa kampeni yake ya mwisho ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, pale Bavaria.

Real Madrid na Barcelona zinaonesha nia ya kumnunua Davies, lakini Ligi Kuu England inaweza kuwa mahali pazuri kwa beki huyo.

Sawa na David, mchezaji huyo wa Bayern atapatikana bila malipo mwishoni mwa msimu wa majira ya joto, lakini kuweka pauni milioni 20 hadi 25 Januari hii kunaweza kumlazimisha kuondoka. Kuna timu kadhaa za Ligi Kuu England zinatafuta beki wa kushoto.

**3. Dani Olmo**
**Klabu zinazomtaka: Arsenal, Man City**
**Ada inayowezekana: Mkopo**

Vita vinavyoendelea vya Barcelona kutaka kumsajili Dani Olmo majira ya joto - ambayo bado hayajatatuliwa licha ya Mahakama Kuu ya Michezo ya Hispania kuamua kuunga mkono - inaacha hatma ya raia huyo wa Hispania hewani.

Akiwa amechangamka tangu kuhamia Katalunya kwa pauni milioni 51, inaonekana hakuna uwezekano kwamba mshindi huyo wa Euro 2024, ataondoka kwenye klabu hiyo kwa mkataba wa kudumu, lakini mkopo unaweza kuidhinishwa kwa kipindi cha pili cha kampeni iwapo msukumo wa Barca kumsajili Olmo utashindwa.

Kuna timu kadhaa za Ligi Kuu England ambazo zingefurahia kuongezwa kwa Olmo kwenye miezi ya mwisho ya kampeni, haswa kwa Arsenal na Manchester City.

**4. Randal Kolo Muani**
**Klabu zinazomtaka: Man Utd, Tottenham, West Ham**
Ada inayowezekana: Mkopo

Randal Kolo Muani amepoteza haraka nafasi ya kupendwa na mashabiki wa Paris Saint-Germain chini ya kocha Luis Enrique na sasa anaonekana kuwa mbali sana na fowadi huyo wa kati mahiri na mwenye kasi aliyekuwa na kiwango cha kuvutia kule Eintracht Frankfurt. Amefunga mara mbili pekee katika mechi 14 akiwa na mabingwa hao wa Ligue 1 msimu huu.

Kuondoka Januari kunaonekana kuwa kuna uwezekano mkubwa na Manchester United na Tottenham zimeonesha nia ya kumsajili mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ufaransa kwa mkopo kwa muda uliosalia wa msimu.

Juventus pia wanamuwania, lakini kivutio cha Ligi Kuu England kinaweza kuwa kishawishi sana kwa Kolo Muani, ambaye anaweza kujijenga upya.

**5. Jonathan Tah**
**Klabu zinazomtaka: Chelsea, Man City, Man Utd**
**Ada inayowezekana: Pauni milioni 12.5**

Huku mkataba wake pia ukimalizika msimu huu wa majira ya joto, Bayer Leverkusen imeripotiwa kuwa tayari kumruhusu Jonathan Tah, mmoja wa wachezaji muhimu wakati wa kampeni yao nzuri ya 2023/24 na anaweza kuondoka pale BayArena kwa pauni milioni 12.5 Januari hii.

Mchezaji huyo wa kati anaweza kufikisha umri wa miaka 29 Februari mwaka huu, lakini yuko katika miaka yake ya kilele na alikuwa karibu sana kujiunga na Bayern Munich msimu wa majira ya joto. Barcelona wameripotiwa kuonesha nia pia.

Chelsea, Man City na Man Utd ni miongoni mwa timu za Ligi Kuu England zinazomsaka beki huyo wa kati kwa sasa na pauni milioni 12.5 ni punguzo la mchezaji wa ubora na uthabiti kama wa Tah.

**6. Douglas Luiz**
**Klabu zinazomtaka: Aston Villa, Man Utd, Man City, Nottingham Forest**
**Ada inayowezekana: Pauni milioni 21**

Douglas Luiz alipata uhamisho wake mzuri kwenda Juventus kutokana na misimu kadhaa ya kuvutia huko Aston Villa. Lakini baada ya miezi sita tu huko Turin, huenda tayari akaonekana si kitu chochote kwa kiungo huyo wa Brazil.

Huku Juventus wakiripotiwa kutaka kurejesha pauni milioni 21 walizotumia msimu wa joto - Luiz anaweza kupatikana kwa ada ya makubaliano.

Kurejea Villa hakutakuwa jambo la maana, wakati Man City, ambayo Luiz aliiwakilisha mapema katika maisha yake ya soka, inaweza kumuona kiungo huyo mkabaji kama mbadala bora wa Rodri kwa kipindi kilichobaki cha msimu.

**7. Marcus Rashford**
**Klabu zinazomtaka: Aston Villa, Tottenham, West Ham**
**Ada inayowezekana: Pauni milioni 35 au mkopo**

Kutoelewana kwa Marcus Rashford na Manchester United kunamaanisha kwamba Januari anaweza kuondolewa pale Old Trafford. Klabu za Italia na Borussia Dortmund zikiripotiwa kuwa mbele ya foleni.

Rashford anaweza kupatikana kwa kitita cha pauni milioni 35, ambacho kitathibitisha ni kidogo kama atarejesha kiwango chake upya. Kutolewa kwa mkopo hadi mwisho wa msimu pia kunawezekana.


West Ham, ambao sasa wananolewa na Graham Potter, ni moja ya klabu zinazomtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, ambaye anaweza kuthibitisha usajili wa busara katika mazingira sahihi.

## Nukuu

"Siku mbili zilizopita Kyle aliomba kuchunguza chaguzi za kwenda kucheza nje ya nchi. Hatuwezi kuelewa klabu ilifanya nini miaka hii bila Kyle. Haiwezekani. Amekuwa beki wetu wa kulia, akitupa kitu ambacho hatukuwa nacho. Lakini sasa akilini mwake, kwa sababu nyingi, angependa kuchunguza kama anaweza kwenda nchi nyingine kucheza miaka yake ya mwisho," **Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola, kuhusu Kyle Walker kuomba kuondoka.**



"Nimekuwa hapa kwa muda. Najua kwamba naweza kupiga hatua kidogo zaidi katika kiwango hicho na nitajaribu kuwasaidia wachezaji wenzangu kwa muda kadri nivezavyo. Mradi nipo uwanjani na nje ya uwanja, nitajaribu kuwasaidia. Unaweza kuona kwamba tulikuwa timu zaidi. Hiyo ndiyo ilikuwa tofauti kubwa," **Beki wa Manchester United, Diogo Dalot, kuhusu maoni ya kocha Ruben Amorim, kumtaka kuongeza ubora zaidi na kuwasaidia wenzake kupiga hatua baada ya kuonesha kiwango cha juu dhidi ya Liverpool, wiki moja iliyopita.**



"Watu walisema wachezaji wa Timu ya Taifa ya Hispania hawataenda kucheza, lakini nilisikia hivyo na nilishangazwa na hilo, kwani huo ni uwongo, Singekataa kuichezea timu ya taifa, napenda kuichezea timu ya taifa. Ni uongo, natumaini hakuna aliyeamini," **Kiungo wa Barcelona, Pedri, akikanusha kuwa wachezaji wa klabu hiyo walifikiria kugomea kuichezea Timu ya Taifa ya Hispania kutokana na mzozo unaohusu usajili wa Dani Olmo.**



# REKODI 5 KALI ZA AHOUA LIGI KUU




AHOUA

**Na Adam Fungamwango**

HACHEZI mpira wa mbwembwe nyingi. Huwezi kumuona anapiga chenga zisizo za lazima, kanzu, matobo, anacheza mpira wa moja kwa moja kusaka matokeo, mpira wa maelekezo.

Kocha Mkuu wa Bravos do Maquis ya Abgola, Mario Soares, amemzungumzia mchezaji huyu, akisema ndiye anayemhusudu zaidi katika kikosi cha Simba.

"Simba ina wachezaji wazuri, ni ngumu kumtaja kila mmoja kwa jina, ila mmoja wao ni yule mwenye jezi namba 10, kwangu huyo ndiyo hatari zaidi, anacheza taratibu tu, lakini mipira yake ni hatari sana," alisema kocha huyo.

Huyu si mwingine ni kijana raia wa Ivory Coast, Jean Charles Ahoua. Amesajiliwa na Simba msimu huu kutoka Klabu ya Stella d'Adjame ya nchini humo, ambapo msimu uliopita alitwaa tuzo ya mchezaji bora wa msimu, MVP.

Ikiwa ni msimu wake wa kwanza tu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, amekuwa na faida kubwa kwa Klabu ya Simba mpaka kumalizika kwa mzunguko wa kwanza.

Ni mchezaji anayebebwa na takwimu zaidi kuliko kufurahisha mashabiki majukwaani.

Hzi ni rekodi tano ambazo tayari ameziweka mpaka kumalizika kwa mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu, timu yake ikiwa imecheza mechi 15 na kuongoza ikiwa na pointi 40.

**1# Kinara wa mabao Simba**

Kwa sasa ndiye kinara wa mabao katika Klabu ya Simba. Amepachika mabao saba, ambayo hakuna mchezaji yeyote wa timu hiyo aliyefikisha idadi hiyo. Kwa muda mfupi tu ameonekana kuizoea Ligi ya Tanzania, pamoja na kuibeba timu yake mabegani mwake.

Mchezaji anayefuatia kwa kufunga mabao mengi kwenye kikosi cha Simba ni Leonel Ateba, akiwa na mabao matano mpaka sasa.

**2# Hatari mabao mguu wa kulia**

Ndiye anayeongoza kwa kupachika mabao kwa mguu wa kulia mpaka sasa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara. Amefunga mabao saba kwa kutumia mguu huo. Kwa sababu amepachika mabao saba mpaka sasa kwenye Ligi Kuu, ina maana yote aliyoyafunga ametumia mguu huo.

Anafuatiwa na Clement Mzize wa Yanga na Selemani Mwalimu wa Fountain Gate, ambao wote wamefunga mabao matano kwa guu la kulia, huku wachezaji sita, Edger Willian wa Fountain Gate, Elvis Rupia wa Singida Black Stars, Paul Peter wa Dodoma Jiji, Feisal Salum na Idd Selemani 'Nado' wote wa Azam na Marouf Tshakei aliyekuwa Tabora United kwa mkopo na sasa amerejea Singida Black Stars, wote hawa wamefunga mabao manne kwa kutumia mguu huo.

**3# Mkali wa penalti**

Ahoua pia anaonekana kuwa na kipaji, uwezo na ufundi wa kufunga mikwaju ya penalti. Achilia mbali kwenye michezo ya kimataifa, kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara amefunga mabao matatu kwa njia hiyo, akiwa mmoja wa wachezaji wanaoongoza kwa mabao hayo.

Wengine ni Ateba wa Simba na Fei Toto, ambao wote wamepachika penalti tatu kila mmoja. Amefunga penalti zote ambazo amepewa kupiga.

Mabao yake aliyafunga kwenye mchezo dhidi ya Dodoma Jiji, Simba ikishinda bao 1-0, dhidi ya KMC, ikishinda mabao 4-0, na dhidi ya JKT Tanzania ikishinda 1-0.

**4# Achuana na Fei Toto kwa 'asisti'**

Anakamata nafasi ya pili kwa kutoa pasi za mwisho kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, akiwa amefanya hivyo mara tano, akizidiwa na Fei Toto mwenye 'asisti' tisa mpaka sasa.

Anaongoza katika klabu yake kwa 'asisti' nyingi zaidi, akifuatiwa na Ladack Chasambi na Mohamed Hussein 'Tshabalala' ambao kila mmoja ana 'asisti' tatu.

**5# Achangia mabao 12, amkaba Fei Toto**

Kiungo mshambuliaji huyo anaongoza kwa kuchangia mabao mengi kwenye klabu yake ya Simba, kwani mabao yake saba na 'asisti' zake tano, anakuwa amechangia jumla ya mabao 12 mpaka sasa, kati ya 31 ambayo timu yake imefunga. Anazidiwa na Fei Toto kwa bao moja zaidi.

Fei Toto amechangia mabao 13 mpaka kumalizika kwa mzunguko wa kwanza, akitoa 'asisti' tisa na mabao manne ya kufunga.

**JE, WAJUA?**



BRENTFORD ndiyo timu pekee kati ya 20 zinazoshiriki Ligi Kuu England, iliyofunga mabao mengi (27), katika mechi 10 ilizocheza uwanja wake wa nyumbani wa Gtech Community, hadi kufikia sasa ligi hiyo ikiwa raundi ya 20.



# Wagonjwa akili wamiminika Mirembe

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

HOSPITALI ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe imesema imepata mafanikio kwa mwaka jana kutokana na ongezeko la watu waliopata huduma ya afya ya akili kufikia asilimia 34.

Hayo yalibainishwa juzi na Mkuu wa Kitengo cha Habari, Mawasiliano na Mahusiano Mirembe, Christian Elias Alais kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Dk. Paul Lawala wakati akitoa tathmini ya hali ya utoaji huduma kwa kipindi hicho.

Alois, alisema ongezeko hilo ni ishara tosha jamii inapata uelewa umuhimu wa magonjwa ya akili ndio maana watu wengi wanajitokeza kupata matibabu hospitalini hapo.

Alisisitiza jamii kuendelea kujitokeza kupata elimu ya afya ya akili ili kusaidia wananchi kupata matibabu sahihi kwa wakati na kupunguza magonjwa ya akili nchini.

Akizungumzia kuhusu eneo la Saikolojia, alisema zaidi ya watu 500 kwa mwaka jana wamehudumiwa ikilinganishwa na wa mwaka juzi 200.

Alisema ongezeko hilo ni sawa na ongezeko la zaidi ya asilimia 75 ikilinganishwa na miaka hiyo miwili.

Alois, alisema kwa mwaka jana, wamehudumia watu zaidi ya 52,000 wa magonjwa yote ikilinganishwa na mwaka juzi 49,000 ambao ni ongezeko la asilimia tano.

Aliwataka wananchi kuendelea kujitokeza kwa wingi kupata huduma katika hospitali hiyo kwa madaktari bingwa wa afya ya akili kwa watoto, vijana na za saikoloijia.

# Ikungi wachangamkia hatimiliki za kimila 760

**Na Thobias Mwanakatwe,** IKUNGI

SERIKALI imetoa hati miliki za kimila zaidi ya 760 kwa Wakazi wa Wilaya ya Ikungi mkoani Singida ili wajikwamue kiuchumi, kuondoa migogoro ya ardhi na mfume dume kwa kuwazuia wanawake kumiliki ardhi.

Hati hizo zilikabidhiwa juzi na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Deogratius Ndejembi kwa wananchi hao.

Ndejembi, alisema hati hizo 762 zitawasaidia, wakazi hao pia kutambua mipaka yao ya ardhi kisheria.

"Mtu akisikia Wizara ya Ardhi anachowaza ni migogoro, tuna kazi kubwa kuhakikisha watu wanakuwa na amani katika ardhi yao," alisema.

Alisema serikali itahakikisha inatafuta fedha kuwawezesha wananchi wengi zaidi kupata hati hizo kwa kuwa ndio njia pekee ya kutatua migogoro ya rasilimali hiyo nchini.

"Tunakwenda kupima vijiji vyote ili kila kijiji kiwe na matumizi bora ya ardhi, tunachotaka ni kuondokana na dhana mtu akisikia neno ardhi, Wizara ya Ardhi anachokiwaza ni migogoro," alisema Ndejembi.

**"Tunaishukuru wizara kuweka miundombinu rafiki kutokana na mipango ya ardhi," alisema.**

Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Thomas Apson, alisema changamoto inayowakabili wananchi ni uelewa mdogo wa sheria ya ardhi na kusababisha kukithiri kwa migogoro baina yao.

Apson, aliwaomba viongozi kuepuka migogoro ya ardhi na kuwaelimisha wananchi namna ya kuondokana nayo.

"Tunaishukuru wizara kuweka miundombinu rafiki kutokana na mipango ya ardhi," alisema.

Awali Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Justice Kijazi, alisema jamii inakabiliwa na tatizo la mila na desturi kandamizi dhidi ya wanawake na wasichana na kuwanyima haki ya kumiliki ardhi.

"Tangu kuanzishwa kwa halmashauri mpaka mwaka 2020 ni asilimia tano pekee ya ardhi inamilikiwa na wanawake," alisema Kijazi.

Alisema katika utekelezaji wa mradi huo, vijiji 12 vya Ikungi vimenufaika na kuvitaja baadhi kuwa ni Kipumbwiko, Wibia, Puma, Samaka na Matongo.



Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana Rushwa nchini (TAKUKURU), Crispin Chalamila akisalimiana na watumishi wa taasisi hiyo mkoa wa Dodoma,wakati wa ziara fupi ya kutembelea ofisi hizo, iliyofanyika mwishoni mwa wiki jijini Dodoma. Kulia kwake ni Mkuu wa TAKUKURU mkoa wa Dodoma,Victor Swella na kushoto kwa Mkurugenzi huyo ni Naibu Mkuu wa TAKUKURU Dodoma, Eugenius Hazina. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# TAKURURU wapewa rungu kutokomeza rushwa

**Na Renatha Msungu** DODOMA

MKURUGENZI Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa nchini (TAKUKURU), Crispin Chalamila amewapongeza watumishi wa taasisi hiyo mkoani hapa kudhibiti rushwa na kuwahimiza kuongeza bidii kuwasaidia wananchi.

Chalamila alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati alipozuru ofisi za taasisi hiyo Mkoa wa Dodoma kuangalia utekelezaji wa majukumu yao.

Alisema katika rushwa, Dodoma wamefanya vizuri na kutaka pongezi hizo kuwa chachu kwenye utendaji wao kukabiliana na rushwa kwa manufaa ya wananchi .

Chalamila, alisisitiza pongezi hizo ziendane na utunzaji siri wa taarifa za wananchi na uchunguzi kujenga imani kwa jamii.

Alisema TAKUKURU ni taasisi muhimu mbele ya jami, hivyo watumishi hao wanatakiwa kutumia nafasi hiyo kutekeleza majukumu yao kwa weledi ili kurahisisha utendaji katika maeneo mbalimbali nchini.

Vilevile, aliwapongeza TAKUKURU Dodoma kwa kutoa elimu kwa wananchi kupiga vita rushwa na kuwahimiza kuendelea na jitihada hizo ili kutokomeza vitendo hivyo katika jamii.

"Nasisitiza jitihada ziongezeke maradufu kwenye utekelezaji wa majukumu ya TAKUKURU," alisema Chalamila.

Mkuu wa TAKUKURU Dodoma, Victor Swella alimshukuru Chalamila kwa kutembelea ofisi hizo na kuahidi wataendelea kufanya kazi kwa ushirikiano ili kuzuia rushwa.

Swella, alitaja moja ya mikakati waliyojiwekea ni kuhakikisha mapambano dhidi ya rushwa yanaendelea kufanyika kwa ushirikiano na wananchi.

# Machifu wapaza sauti ukatili wanawake, watoto nchini

**Na Peter Mkwavila,**DODOMA

KATIBU wa Baraza la Machifu Mkoa wa Dodoma, Ndahani Chinang'anang'a, ameiomba serikali kuwachukulia hatua watu wanaojihusisha na ukatili na mauaji ya watoto, wanawake na walemavu ili vitendo hivyo vitokomezwe katika jamii.

Chinang'anang'a, alitoa ombi hilo juzi jijini hapa katika kikao kilichoandaliwa na Taasisi ya Wafikiriaji Duniani (TAWADU).

Alisema serikali inapaswa kuchukua hatua kali kukomesha vitendo hivyo kwa kudhalilisha wanawake na watoto na mauaji ya watu wasiokuwa na hatia.

Alisema vitendo hivyo vimekuwa vikirudisha nyuma ukuaji wa uchumi na maendeleo, hivyo jamii inatakiwa kuhakikisha wahusika wanawajibishwa.

Aliwataka machifu kutoa elimu ya maadili kwa jamii na kutatua migogoro ya ardhi, ndoa na mmomonyoko.

Chifu wa Mkoa wa Dodoma, Yasin Ally Bilingi, aliwataka wananchi kudumisha amani na utulivu katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi mkuu utakaofanyika nchini mwaka huu.

Mlezi wa baraza hilo, Mohamed Keba, alikemea ufanyaji kazi kwa mazoea, akisema umesababisha kupuuzwa tamaduni, mila na desturi nchini .

Katibu Mkuu wa TAWADU, Mayalla Mayalla, alisema wataendelea kupinga vitendo vya uvunjifu wa amani katika jamii kwa kushirikiana na mamlaka husika.





# Mifugo yafa kwa kunywa sumu

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WAFUGAJI wa Kijiji cha Mlima Njiwa kilichopo wilayani hapa Mkoa wa Mbeya, wameingiwa na hofu ya uchumi wao kuporomoka baada mifugo yao kuanza kufa kwa madai ya kunywa maji yenye kemikali za sumu yanayodaiwa kutiririshwa kutoka kwenye mitambo ya kuchenjulia dhahabu.

Hofu hiyo iliibuka mwishoni mwa wiki iliyopita baada ya zaidi ya ng'ombe 12 wanaomilikiwa na wafugaji jamii ya Wamasai kudaiwa kufa papo hapo kwa kunywa maji kutoka kwenye moja ya mitambo hiyo.

Wafugaji hao walidai kuwa hali hiyo pia inahatarisha maisha yao kutokana na maji hayo kutiririka kwenye vyanzo vya maji wanayotumia kwa matumizi ya nyumbani.

Mmiliki wa ng'ombe hao, Juma Kibuda alidai kuwa tukio hilo ni la pili kwa mifugo yake kufa kwa kunywa maji hayo kutoka kwenye mitambo hiyo na kuiomba serikali kuwadhibiti wamiliki wa mitambo hiyo.

Kibuda, alidai amepata hasara ya zaidi ya Sh. milioni 12 kutokana na ng'ombe hao kufa.

"Hili tukio limekuwa la pili, kuna wakati ng'ombe na mbuzi wangu walikufa, mmiliki anashindwa kudhibiti maji haya yasitiririke, tumewaita wataalamu wamekuja wakathibitisha ni sumu kwahiyo hii ni hasara kwangu," alilalamika Kibuda.

**"Tunaomba serikali itusaidie. Hapa mwenzetu amepoteza mifugo, madhara yanaweza yakawa makubwa zaidi kwa binadamu na viumbe wengine," alisema Ole Rapoy.**

Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji Wilaya ya Chunya, Shang'ai Ole Rapoy, alidai kipindi cha kiangazi maji hayo yenye sumu yalikuwa hayatiririki kwenda mtoni na kwamba tatizo hilo limeibuka baada ya mvua kuanza kunyesha.

Rapoy, alidai maji ya mvua yalifurika kwenye mabwawa kutoka kwenye mitambo hiyo na kusafirisha sumu kwenda mtoni ambako ndiko ng'ombe wanakunywa maji. Alisema kwenye mto huo ambao sumu hizo zilitiririka kuna viumbe wengine wanaoishi ambao nao maisha yao yako hatarini.

"Tunaomba serikali itusaidie. Hapa mwenzetu amepoteza mifugo, madhara yanaweza yakawa makubwa zaidi kwa binadamu na viumbe wengine," alisema Ole Rapoy.

Mmoja wa wafugaji wa eneo hilo, Elisha Kimanga, alidai tukio la mifugo kufa kwa sababu ya kunywa maji ya sumu ni la tatu kutokea katika eneo hilo.

Aliwaomba wamiliki wa mitambo hiyo kuzingatia maisha ya wananchi na viumbe wengine na serikali kukagua mara kwa mara maeneo ya kuchenjulia dhahabu ili kuhakikisha sumu hazitiririshwi hovyo.

Mmiliki wa mitambo inayodaiwa kutiririsha sumu hiyo, Taifa Mlekwa alisema tatizo hilo linasababishwa na mwingiliano wa shughuli zake za uchimbaji wa madini na ufugaji mara kwa mara. Mlekwa, alisema eneo hilo analitumia kwa ajili ya kuchimba dhahabu na kuchenjua, lakini kuna wafugaji wanaingiza mifugo na kuchungia na kusababisha migogoro.

"Wakati mwingine unakuta mbuzi wameingia humu, wanakunywa maji na wanakufa, ikitokea hivyo tunakaa mezani na kumaliza tatizo, sasa mara nyingi nimekuwa nikiongea nao wasiingize mifugo hawaelewi," alisema Mlekwa.

Ofisa Mifugo wa Wilaya ya Chunya, Dk. Benedict Nyamatogo aliwakutanisha mmiliki wa mifugo hiyo, Mmiliki wa mitambo na viongozi wa Kijiji cha Mlima Njiwa kwa lengo la kuwapatanisha ili kuepusha visasi kuibuka.

Nyamatogo, alisema baada ya kusikiliza pande zote mbili walifikia mwafaka na kuwahimiza kuendelea kushirikiana.

*Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz*

## Wakulima 'walia' kushindwa kusafirisha pembejeo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI wa Kata ya Ilungu wilayani hapa Mkoa wa Mbeya wameiomba Serikali kukarabati barabara ili kuwarahisishia usafirishaji wa pembejeo kwenda mashambani.

Wakizungumza na Nipashe, wakazi hao, walisema kuwa serikali kupitia Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) imekuwa ikikarabati barabara hizo mara kwa mara lakini kipindi hiki hali mbaya ni kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha.

Mkazi wa Kijiji cha Ifupa, Leonard Mwayonga, alisema barabara hizo zimeharibika na kugeuka makorongo na kusababisha wenye magari kusitisha usafiri na kukwamisha juhudi zao kwa kushindwa kufikisha pembejeo mashambani.

"Huku tunalima viazi kwa wingi na msimu huu tunapeleka mbolea kwa ajili ya kukuzia viazi na mahindi, sasa hali hii ya makorongo kwenye barabara hizi hata pikipiki zinapita kwa shida," alisema Mwanyonga.




Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Kheri James akimpongeza mmoja kati ya watu 25 waliokabidhiwa vitendea kazi na Mradi wa Feed The Future kwa ajili ya kwenda kuongeza thamani ya kilimo na ufugaji jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Kamati yajitosa mgogoro wa wakulima, serikali

**Na Nebart Msokwa,** SONGWE

KAMATI ya Ulinzi na Usalama Wilaya ya Songwe mkoani hapa imeingia kati mgogoro baina ya wakulima wa tumbaku wa Kata ya Gua kuzuiliwa na Serikali kulima zaidi ya ekari 50 za zao hilo.

Kamati hiyo ikiongozwa na Mkuu wa Wilaya hiyo, ilifanya ziara katika eneo hilo mwishoni mwa wiki kwa lengo la kuwasikiliza wakulima hao na kutafuta suluhu ya mgogoro unaofukuta baada ya kuzuiwa kuendelea na kilimo hicho.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya ziara hiyo, Mkuu wa Wilaya hiyo, Solomon Itunda, alisema hawakufanya maamuzi yoyote na badala yake waliamua iundwe kamati huru ya kuchunguza chanzo cha mgogoro huo.

Itunda, alisema wameamua kuunda kamati hiyo ya wadau wakiwemo maofisa wa vyombo vya ulinzi na usalama, wananchi na wataalamu kutoka Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo ya Songwe.

Alisema maofisa wengine watakaounda timu hiyo wanatoka Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS).

Alisema mgogoro huo umeibuka baada ya wakulima hao kubainika kuvamia hifadhi ya msitu huo wa nyuki na kuendesha kilimo cha tumbaku na kusababisha uharibifu wa mazingira. "Msingi wa ziara yetu ilikuwa ni kujiridhisha na taarifa zinazoonesha baadhi ya wananchi wanafanya shughuli za kilimo katika maeneo hayo ya hifadhi kinyume na sheria, lakini tulichokibaini hatuwezi kutolea maamuzi mpaka wataalamu watusaidie," alisema Itunda.

Hata hivyo, alisema timu hiyo itatembelea maeneo yanayolalamikiwa ili kujiridhisha kisha kuandaa taarifa ambayo itatumika kutoa maamuzi ya mwisho.

Alisema itatakiwa kufanya kazi ndani ya siku mbili ili maamuzi yafanyike haraka wakati msimu wa kilimo haujakwisha.

Baadhi ya wakulima waliomba serikali kukamilisha uchunguzi mapema ili waendelee na msimu wa kilimo na kunusuru vyama vyao vya ushirika kufa kwa kukopesha pembejeo.

Walidai wameotesha mbegu kwa ajili ya kupanda na kununua mbolea, lakini serikali imewazuia na kuhatarisha uhai wa vyama vyao vya msingi.

Mwenyekiti wa Chama cha Msingi cha Wakulima wa Tumbaku cha Gua (Gua AMCOS), Elias Dereva, alisema wakulima wanaoathirika na katazo hilo ni zaidi ya 80 kutoka vyama vitatu vya msingi vilivyopo kwenye kata hiyo.

Dereva, alisema baadhi ya wakulima wamelima mashamba yao na kuathiriwa na katazo hilo.

Bathoromeo Kyando, mmoja wa wakulima hao, alisema tangu walipozuiliwa kuendelea na kilimo kwenye mashamba hayo hawaelewi cha kufanya na kwamba matumaini yao yamebaki kwa timu hiyo.

Gua ni miongoni mwa kata tatu za wilaya hizo zinazalisha tumbaku kwa wingi na ndilo zao kuu la biashara kwa wakazi wa eneo hilo.



## Vijana kuzalisha tani 8,400 mbegu za mahindi

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

AWAMU ya pili ya Mradi wa Jenga Kesho Iliyobora (BBT), inatarajia kuzalisha tani zaidi 8,400 za mbegu bora ya mahindi aina ya C105 kwenye shamba la ekari 4,200 la Ndogoye lililopo Chamwino mkoani hapa.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi Msaidizi Mipango na Bajeti wa Wizara ya Kilimo, Mohamed Chikawe wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya mapokezi ya vijana wanufaika wa mradi huo kutoka mikoa mbalimbali nchini.

Chikawe, alisema katika shamba hilo wanatarajia kupokea vijana 420, kila mmoja atakabidhiwa ekari 10 kwa ajili ya kuzalisha aina hiyo ya mbegu kwa ajili ya kutumika katika msimu ujao wa kilimo.

"Mpaka sasa tumepokea vijana 209 na bado wanaendelea kuwasili ili kufikia idadi hiyo ya vijana katika shamba hilo ambalo ni awamu ya pili ya kuwasili," alisema.

Alifafanua kuwa vijana hao wanakwenda kuzalisha mbegu hizo kwa usimamizi wa wataalam wa kilimo kutoka taasisi za uzalishaji mbegu bora nchini.

Mmoja wa vijana hao, Fanuel Buu kutoka Wilaya ya Babati mkoani Manyara, aliishukuru serikali kwa kutoa fursa za kilimo kwa ajili ya vijana nchini.

Buu, alisema fursa hizo zinachangia kupunguza uhaba wa ajira kwa vijana na kujiandaa na maisha yao ya badaye.

"Vijana tunapopata fursa kama hizi tuzichangamkie ili zitusaidie kujiinua kiuchumi ikiwemo kujiajiri badala ya kusubiri ajira kutoka serikali na watu binafsi,"alisema.

Ilumbo Yohana kutoka wilayani Chamwino Mkoa wa Dodoma, alisema wanakwenda kutumia fursa hiyo ya kilimo iliyotolewa na serikali kwa vijana kujiingizia kipato na kukuza uchumi wa taifa kupitia sekta ya kilimo.

Yohana, alisema kwa sasa kilimo ni fursa kubwa kwa vijana kutokana na serikali kuwekeza, hivyo wanapaswa kuchangamkia na kuondokana na umaskini.

# Mapinduzi yashusha neema kiuchumi, kibiashara

**Na Rahma Suleiman,** PEMBA

KUFANYIKA kwa Sherehe za Miaka 61 kisiwani hapa kumefungua fursa za biashara na uchumi kwa wananchi kutokana na mamia ya watu kutoka nje kuhudhuria sherehe hizo.

Kumiminika kwa idadi kubwa ya watu kisiwani hapa kumesababisha baadhi ya huduma kukosekana ikiwemo nyumba za wageni baada ya kujaa wateja.

Wakizungumza na Nipashe, baadhi ya wakazi wa kisiwani hapa, walisema wafanyabiashara wa nyumba za wageni wameitumia fursa hiyo kupandisha bei za malazi kwa siku kutoka Sh. 50,000 hadi Sh.70,000.

"Tangu Januari ilivyoanza wageni wengi wameanza kumiminika Pemba, kwa siku hizi za mwisho kufikia kilele cha Miaka 61 ya Mapinduzi Pemba imefurika watu, jambo ambalo kwa upande mmoja ni fursa nzuri kwa wafanyabiashara ikiwemo wanaouza vyakula" alisema Hamad Ali, Mkazi wa Chakechake Pemba.

Ali, alisema mzunguko wa fedha nao umeongezeka kutokana na watu kuwa na mahitaji makubwa ya huduma.

Ali Bakari, mfanyabiashara wa supu ya Pweza eneo la Machomane, alisema kutokana na ongezeko la watu kisiwani hapa kwa sherehe hizo, hali ya biashara ni nzuri kwa sababu wateja wameongezeka.

> **"Kabla ya huu ugeni uliofika kisiwani hapa biashara yangu ilikuwa imedoda, wateja hawakuwa wengi kama sasa kwa kweli fursa ya kufanyika sherehe hizi Pemba ni neema kwa wafanyabi-**

"Kabla ya huu ugeni uliofika kisiwani hapa biashara yangu ilikuwa imedoda, wateja hawakuwa wengi kama sasa kwa kweli fursa ya kufanyika sherehe hizi Pemba ni neema kwa wafanyabiashara," alisema.

Alisema ili biashara ikue inahitaji mzunguko wa fedha na watu wanapokuwa wengi matumizi nayo yanaongezeka kwa sababu ya kuwepo kwa mahitaji mbalimbali.

Kwa upande wa usafiri wa meli na ndege kutoka Unguja hadi Pemba kwa siku ya Januari 11 na 12, wasafiri waliongezeka. Katika hali isiyo ya kawaida katika Bandari ya Malindi Mjini Unguja, boti tano zilifanya safari zake kwa wakati mmoja kutoka Unguja kwenda Pemba.

Wengi wa abiria katika boti hizo ni wageni waliohudhuria sherehe hizo za Mapinduzi zilizofanyika katika Uwanja cha Gombani.

Hawakukosea wahenga waliosema kuwa kwenye msafara wa mamba, kenge nao hawakosekani baada ya baadhi ya madalali wa tiketi za boti kuibuka na kuuza kinyume na sheria.

Madalali hao waliandisha bei kwa kuuza tiketi kutoka Sh. 20,000 hadi Sh 30,000.

Uchunguzi wa Nipashe ulibaini kuwepo kwa vitendo vya udanganyifu huo kwa abiria kuuza tiketi kwa bei kubwa ya Sh.30,000 wakati zikiwa zimeandikwa kwa bei elekezi ya serikali ya Sh.20,000 huku zikiwa hazina majina ya abiria husika.



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum Dk.Dorothy Gwajima kushoto akikagua ujenzi wa madarasa mpya ya Shule ya Msingi Langoni iliyopo Ulyankulu mkoani Tabora, katika ziara yake ya kikazi mkoani humo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 5,000 waathiriwa dawa za kulevya Z'bar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

ZANZIBAR inakadiriwa kuwa na watu zaidi ya 5,000 walioathiriwa na matumizi ya dawa za kulevya.

Takwimu hizo zimetolewa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harusi Said Suleiman wakati akizungumza na makundi ya vijana na wanawake kwenye huduma ya tiba kurekebisha tabia na kuachana na matumizi ya dawa za kulevya katika Kituo cha Kidimni Wilaya ya Kati Unguja.

Alisema dawa za kulevya ni janga la taifa na kwamba limeathiri kundi kubwa la vijana kwa kupoteza ajira na uaminifu katika familia.

Alisema inakadiriwa zaidi ya watu 5,000 visiwani Zanzibar wameathiriwa na dawa za kulevya na wanahitaji kupata tiba ili kuondokana na tatizo hilo moja kwa moja.

"Tumefungua kituo cha kimataifa kwa ajili ya kurekebisha tabia kwa vijana kuachana na matumizi ya dawa za kulevya," alisema Waziri huyo.

Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Kupambana na Dawa za Kulevya Zanzibar, Burhani Zubeir Nassor, alisema kufunguliwa kwa kituo hicho kutoa huduma kwa makundi ya watu walioathirika kwa dawa za kulevya ni jambo jema.

Alisema kumekuwepo na mafanikio makubwa kwa kituo hicho kurekebisha tabia kwa baadhi ya vijana baada ya kupata tiba sahihi.

"Tumepata mafanikio ambapo zaidi ya vijana 200 tumewapatia tiba na kuacha moja kwa moja kutumia dawa za kulevya na kurudi katika ngazi za familia," alisema.

Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Mariyam Juma Sadalla, alisema serikali imejenga kituo hicho kwa gharama ya zaidi ya Sh. bilioni saba kwa ajili ya kurekebisha tabia kwa vijana kuachana na matumizi ya dawa hizo.

Mariyam alitaja faida za kituo hicho kuwa ni vijana kufundishwa ujasiriamali na kutumia ujuzi huo uraiani baada ya kuachana na matumizi ya dawa hizo.

*Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz*

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA VYETI



**AZIFA ISSA LICHUMBU** anatangaza kupotea kwa cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye index No. **S3981/0007** Kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **SABODO SECONDARY SCHOOL** mwaka **2018,** Cheti cha kidato cha nne chenye index No. P5014-0006 Killchotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **PADUCAH SECONDARY SCHOOL CENTRE** mwaka 2019. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/60268/2024**

## KUPOTEA KWA VYETI



**SAIDI FADHILI MKUYAWA** anatangaza kupotelewa na cheti cha darasa la saba kilichotolewa na SHULE YA MSINGI TAMBANI mwaka 2018. Cheti cha kidato cha nne chenye index namba S2257-0115 kilichotolewa na SHULE YA SEKONDARI KITONGA mwaka 2022. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Control number: **9910842373905.**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**HYTHAM ALLY KAVIRA** naomba kutangaza kupoteza Hati yangu ya Kusafiria yenye namba TAE087486 iliyotolewa tarehe 05/02/2019 na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. **Taarifa ya polisi: PHQ/DAR/KIG/8455/2025**

## KUPOTEA KWA CHETI



**JOHN SOLOMONI MADAHA,** Anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye Index namba S0172/0026 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia shule ya Don Bosco Seminary Mwaka 2018. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha Polisi.

**TAARIFA YA POLISI: DOM/DOD/RB/884575/2020**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**HARID KASSIMU MAYUHANA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T.590 DJM.** YEYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU NAE. TAARIFA YA POLISI **PHQ/MBE/MBE/1622/2025.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**ELIYA BLASIO KAJORO** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI AINA YA SANLG YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 880 ENJ.** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHO KARIBU. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/SHI//KAH/11345/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MATEKELEZA CHANG'A AND COMPANY LIMITED** WANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA **LAND CRUISER PICK UP** YENYE USAJILI **T372 DDP** KWA YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA KADI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA **PHQ/IRI/MUF/631/2025.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA BAJAJI

**JAPHET KASIRI MTYAMA**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili MC **707 BTN** Chasses Namba **MD6M14PK9H4E79080**, Engine Namba **0K4DH4499249.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Polisi Taarifa: **PHQ/KIL/MOS/986/2025**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI NA BAJAJI

**NORBERTH SAMWEL SUMKA**

ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI NA BAJAJI ZENYE USAJILI T499 DLP, MC 759 BXA, MC 342 CCE KWA YEYOTE ATAEFANIKIWA KUZIONA KADI HIZO ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI **TAARIFA PHQ/IRI/IRI/635/2025.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ALPHONCE LUKUMBUZYA MAGAMBO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 287 DPZ – TOYOTA IST.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/9250/2025.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**JOSEPH RICHARD SANGA**

anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye namba za usajili MC 424 BCN aina ya BAJAJ. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DAR/UBU/8696/2025**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**MARIAM MWAKASEGE MWANKUSYE**

anatangaza kupotelewa na kadi za pikipiki zenye usajili namba **T.307 CHQ-TOYO, MC.211 CEE-WANHOO, MC.368 CFC-PIAGIO, MC.130 CLU-KINGLION na MC.777 CRD-KINGLION.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake. Taarifa ya polisi: **PHQ/SHI/KAH/458/2025.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya KILOMBERO**
**Kituo cha MKAMBA Mkoa wa MOROGORO**
**Shauri la Ndoa No. 2/2025**
**Jina la Mdai: MARIAM MAMDALI MSUYA**
**Jina la Mdawa: ROBERT SINGANO MTANGI**

### KUITWA SHAURINI MDAIWA

**(Kanuni ya 18 ya kanuni za utaratibu wa Madai katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa: ROBERT SINGANO MTANGI**

**Kwa kuwa mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kamba MADAI YA TALAKA KWASABABU YA UKATILI WA KIMWILI NA KIHISIA**

Hivyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya JUMANNE tarehe 21 mwezi 01 mwaka 2025 saa 3 Asubuhi/mchana na kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujieleza.

**ANGALIZO:** Kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikathibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 10 Mwezi 01 Mwaka 2025.

HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO MKAMBA WILAYA YA KILOMBERO


**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO,MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## OCHA yaonya kuzorota hali ya kibinadamu Kivu

**KIVU,** DRC

TUME ya Umoja wa Mataifa inayoshughulika na masuala ya kibinadamu (OCHA), imetahadharisha kuwa, hali ya kibinadamu inaendelea kuwa mbaya katika jimbo la Kivu Kaskazini, kunakoshuhudiwa vita kati ya jeshi la FARDC na waasi wa M23.

Mkuu wa tume hiyo Bruno Lemarquis, alitoa kauli hii, baada ya ripoti kuwa vita vinavyoendelea vimesababisha watu zaidi ya 100,000 kuyakimbia makazi yao ndani ya siku 10 zilizopita.

OCHA ilisema, watu hao wamekimbia makazi yao tangu Januari mosi mwaka huu wakati vita, vilipoanza katika wilaya ya Masisi.

Umoja wa Mataifa (UN) ulitoa wito wa kukomesha machafuko na mashambulio dhidi ya raia na wafanyakazi wa kutoa misaada kuruhusiwa kuwafikia watu wenye uhitaji wa chakula, maji na dawa.

Wakati hayo yakijiri, jeshi la serikali linaloshirikiana na wapiganaji Wazalendo, lilisema, limefanikiwa kudhibiti tena mji wa Ngungu, Kaskazini mwa Masisi uliokuwa umechukuliwa na waasi wa M23.

Msemaji wa Jeshi Kivu Kaskazini, Luteni Kanali Guillaume Kaiko, alisema maofisa wa usalama wanafanya kila linalowezekana, kuhakikisha kuwa wananchi wanaishi kwa amani. **RFI**

## Maofisa usalama 21 wauawa Nigeria

**ABUJA,** Nigeria

NCHINI Nigeria, maofisa 21 wa usalama, wanaoshirikiana na Jeshi la Nigeria wameuawa baada ya kushambuliwa kwa kushtukiza na watu wenye silaha, katika jimbo la Kaskazini Magharibi mwa jimbo la Katsina.

Ilielezwa kuwa shambulio hilo lilitokea wakati maofisa hao wa usalama, walipokuwa wanarejea katika kambi yao, baada ya kuhudhuria msiba wa mwenzao, aliyeuawa na watu wenye silaha katika kijiji cha Baure, wilaya ya Safana.

Msemaji wa polisi katika eneo hilo Abubakar Aliyu alisema jana kuwa maofisa hao wa usalama wa serikali, walipigwa risasi katika shambulio hilo, na jitihada zinaendelea kuwatafuta waliohusika, katika tukio hilo lililotokea siku chache zilizopita.

Ilielezwa kuwa Jimbo la Katsina, ni miongoni mwa maeneo yanayopatikana Kaskazini Magharibi mwa Nigeria, ambayo hushuhudia mashambulio ya mara kwa mara ikiwemo utekaji watu.

Magenge yenye silaha hujificha katika misitu ya Zamfara, Katsina, Kaduna na Niger na kusababisha hata shule kufungwa kwa hofu za kiusalama. **RFI**

# Baba avunja kiuno akisherehekea ufaulu wa mwanae

**NAIROBI,** Kenya

BABA wa kijana Nathan Kipng'eno amedaiwa kuvunjika kiuno wakati akisherehekea kutokana na furaha iliyopitiliza baada ya mwanae kupata ufaulu mzuri wa daraja A katika mtihani wake wa mwisho wa shule ya upili nchini Kenya.

Ilielezwa kuwa baba huyo hakuweza kuzuia furaha yake tele baada ya matokeo bora ya mwanawe, hali iliyosababisha kuruka kwa nguvu na kucheza kwa furaha huku akimuacha mwanaye katika kicheko walipokuwa wakisherehekea habari hizo nyumbani.

Ilielezwa kuwa Babake Nathan alikuwa amevua kanzu yake ili kucheza huku akionesha kiburi chake baada ya kufaulu vizuri kitaaluma kwa mwanawe.

Katika hatua nyingine, watumiaji wa mitandao ya kijamii walibaini furaha ya baba huyo walipokuwa wakielekea sehemu ya maoni kuitikia video hiyo.

Mtumia mtandao aliesomeka kama Shule ya Jumuiya ya Jabes, aliandika kuwa "huyo ni mzazi wa kawaida wa Kenya aliyeelemewa na kulea familia yake pendwa anapoona juhudi zake kuwa maua. Lazima afurahi."

Kanisa la City of Joy, aliandika "Hongera sana! Mungu akulinde kwa viwango vya juu zaidi. Mithali 15:20 inasema mwana mwenye hekima humfurahisha baba yake."

Jebongi Junior aliandika "Ninamshukuru sana kaka yangu mdogo Nathan Kipng'eno ametufanya tujivunie, tunamshukuru Mungu kwa matendo mema kwetu. Hongera sana, Kipng'eno Nathan."

Katika chapisho la nostalgic, alishiriki kumbukumbu kutoka 2015, akisisitiza nguvu ya ahadi, bidii, na kujifunza maisha yote.

Ujumbe wake wa kihisia, unaorejea ushauri wa baba yake usio na wakati juu ya thamani ya kusoma, ulionesha athari ya mabadiliko ya elimu na msaada wa wazazi. **KTN**



Raia katika mji wa Port Sudan wakisherehekea ushindi wa jeshi la Sudan dhidi ya RSF baada ya kufanikiwa kurudisha mji wa Wad Madani, uliotekwa na wanamgambo wakati wa vita vilivyokuwa vinaendelea Sudan. **PICHA: MTANDAO.**

# Jeshi Sudan larejesha mji wa Mashariki

**KHARTOUM,** Sudan

JESHI nchini Sudan limesema kuwa limeuteka mji muhimu mashariki mwa nchi hiyo, moja ya mafanikio yake makubwa katika vita vya karibu miaka miwili dhidi ya vikosi vya waasi.

Picha kwenye mitandao ya kijamii zilionesha watu wakisherehekea barabarani huku wanajeshi wakiingia katika mji wa Wad Madani.

Kiongozi wa kundi la wanamgambo la Kikosi cha Msaada wa Haraka (RSF), Jenerali Mohamed Dagalo, alikiri hasara hiyo katika ujumbe wa sauti.

Ilielezwa kuwa kukiri kwake kulikuwa na hasira na mbwembwe, akihusisha kushindwa kwa jeshi la anga la juu na matumizi ya ndege zisizo na rubani zilizotengenezwa na Iran.

Lakini aliapa kuendelea kupigana hadi ushindi, hata kama itachukua miaka 20 zaidi.

Wad Madani ni mji mkuu wa jimbo la Al Jazira, na uko kilometa 40 kusini mwa mji mkuu wa nchi hiyo, Khartoum.

Ilielezwa kuwa ghasia zilizuka kati ya jeshi na RSF mwezi Aprili 2023 kufuatia siku za mvutano huku wanachama wa RSF wakisambazwa nchini kote katika hatua ambayo jeshi liliona kama tishio.

Vita hivyo vimegharimu maelfu ya watu, na kwamba katika kile ambacho Umoja wa Mataifa (UN) umekiita mojawapo ya migogoro mikubwa zaidi ya watu kuhama makazi duniani, ambako takriban watu milioni tisa walilazimika kuyahama makazi yao.

Maofisa wa umoja huo walisema nchi hiyo pia inaingia kwenye baa la njaa, huku watu milioni 24.6 karibu nusu ya watu wanaohitaji msaada wa haraka wa chakula.

Mapema mwezi huu, Marekani ilimuwekea vikwazo kiongozi wa RSF Dagalo baada ya kulishutumu kundi hilo kwa kufanya mauaji ya halaiki.

Maofisa walisema alikuwa anaadhibiwa kwa jukumu lake katika ukatili wa kimfumo dhidi ya watu wa Sudan wakati wa mzozo wa miezi 20. **BBC**

# MORRISON, MIQUISSONE KUANDALIWA TAMASHA LA UTAMBULISHO KENGOLD

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya KenGold, imesema inatarajia kuwatambulisha wachezaji wapya iliyowasajili kipindi cha dirisha dogo la usajili, akiwamo Benard Morrison kwa tamasha kubwa.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Jose Mkoko, jana kwa mara ya kwanza amekiri kuwa klabu hiyo imemsajili Morrison, akisema pia wamefanya usajili wa wachezaji wengine wenye majina makubwa, kutoka Zambia, Msumbuji, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na Tanzania.

Ingawa hakutaka kuwataja wachezaji iliyowasajili, taarifa zinaeleza kuwa klabu hiyo ipo katika mazungumzo na winga wa zamani wa Simba, Luis Miquissone, Thadeo Lwanga, Obrey Chirwa, Rally Bwalya na wengineo.

Mkoko amesema tamasha hilo limepewa jina la Makarasha Day, ambalo litafanyika jijini Mbeya na lengo ni kuwatambulisha wachezaji iliyowasajili.

"Tumeandaa tamasha la kuwatangaza wachezaji wetu, unawasajili wachezaji kama Morrison halafu umtangaze hivi hivi tu wakati alicheza na kuitikisa Tanzania, haiwezekani.

"Pia kuna wachezaji kutoka nje ya Tanzania ambao hawajacheza hapa, nao tutawatangaza, wanatoka Msumbiji, Zambia, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, unawatambulishaje bila tamasha? Tamasha letu litaitwa 'Makarasha Day,'" alisema Mkoko.

Alisema wamefanya usiri mkubwa kwenye usajili wao ili kulipa thamani tamasha lao, kwani mashabiki watataka kuwaangalia wachezaji waliowasajili ambao wengi wao walicheza Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mafanikio makubwa.

"Hata huu usajili wa Morrison, tulitaka uwe 'sapraizi', lakini ulivuja kwa sababu alionekana na Mkurugenzi wa Klabu, Kenneth Mwakyusa, kwenye Uwanja wa Songwe, kwa hiyo rasmi leo natangaza kuwa ni kweli Morrison ni mchezaji halali wa KenGold, na atakwenda kutupa nguvu kuelekea mzunguko wa pili, wengine bado ni siri, baadhi tumemalizana nao, baadhi tunakwenda kumalizana nao muda si mrefu, wote tutawatangaza kwenye Makarasha Day," alisema.

## Matano, Amri 'Stam' waahidi kuipaisha Fountain Gate FC

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Robert Matano, na msaidizi wake, Amri Said, wameahidi kuifanya Fountain Gate kuwa tishio kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara hususan mzunguko wa pili utakapoanza.

Wakizungumza jana baada ya kutambulishwa rasmi juzi, makocha hao wamesema ingawa Fountain Gate haijafanya vibaya sana kwenye ligi hadi kumalizika kwa mzunguko wa kwanza, lakini wanatarajia kuifanya imara zaidi, huku pia ikiwa timu isiyoruhusu ovyo mabao.

Siku chache zilizopita, gazeti hili liliandika kuhusu klabu hiyo kuwa mbioni kumtangaza kocha Matano raia wa Kenya kuchukua nafasi ya Mohamed Muya aliyetimuliwa baada ya kumalizika kwa mchezo wa Ligi Kuu kati ya timu hiyo dhidi ya Yanga, uliochezwa Desemba 29, mwaka jana, na kubugizwa kwa mabao 5-0, kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam.

"Kwanza nashukuru kuwa hapa, nimeifuatilia kwa muda Fountain Gate, ni timu nzuri na inataka kuendelea, na hizi ndiyo zangu, kuzitoa timu chini kuzipeleka juu, ni changamoto kubwa kwangu kwa sababu sijawahi kufundisha nje ya nchi ya Kenya, niko tayari kwa kazi, naahidi kuifanya kuwa tishio kwenye Ligi Kuu," alisema kocha huyo.

Klabu hiyo pia ilimtambulisha beki wa kati wa zamani wa Simba, Amri 'Stam', kuwa kocha msaidizi, ambaye naye alisema amekuja kuiwezesha timu hiyo kutimiza malengo inayoyakusudia.

"Mimi nimefurahi sana kujiunga na timu hii, naahidi nitaitoa hapa ilipo na kuipeleka kwenye malengo ya klabu inapotaka, matokeo ya timu hayakuwa mabaya sana, ila tutaboresha hasa sehemu ya ulinzi," alisema Amri ambaye alikuwa Kocha Mkuu wa Klabu ya KVZ ya Zanzibar.

Kocha Matano amezifundisha Klabu za AFC Leopards, US Nakuru, Sofapaka FC na Tusker zote za Kenya, akiwa na vikombe 11 vya Ligi Kuu ya Kenya.

Hadi kumalizika kwa mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Fountain Gate inakamata nafasi ya sita kwenye msimamo wa ligi, ikiwa na pointi 20, lakini rekodi yake mbaya ni kuwa ndiyo timu iliyoruhusu mabao mengi mpaka sasa kwenye ligi, ikiruhusu 32 mpaka sasa.

## UNAPITAJE HAPA? ...



Beki wa kulia wa Al Ahly ya Misri, Khaled Abdelfattah (kushoto), akimthibiti kiungo wa Stade d'Abidjan ya Ivory Coast, Mohamed Niampa, kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika iliyopigwa nchini Ivory Coast juzi na kumalizika kwa wageni kushinda mabao 3-1. **PICHA: MTANDAO**

## Serikali yatoa maagizo TPBRC

**Na Shufaa Lyimo**

SERIKALI imeitaka Kamisheni ya Ngumi za Kulipwa Tanzania (TPBRC) kuhakikisha bondia atakayecheza ngumi za kulipwa lazima awe amecheza ngumi za ridhaa hapa nchini.

Agizo hilo lilitolewa jana na Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamis Mwinjuma maarufu Mwana FA, katika kikao cha pamoja na mapromota kilichofanyika jijini Dar es Salaam.

Alisema anataka kuona wakiweka utaratibu wa mabondia kucheza mapambano kadhaa ya ngumi za ridhaa ndipo wacheza yale ya kulipwa.

"Hivi sasa mabondia wengi wanaingia moja kwa moja kwenye ngumi za kulipwa bila kupitia ngumi za ridhaa , hivyo TPBRC nahitaji kupata majibu Januari 15, mwaka huu, ni mapambano mangapi wanatakiwa kupitia," alisema Mwinjuma.

Waziri huyo aliwataka mapromota kuhakikisha wanakuwa na ripoti ya afya kwa mabondia kabla ya kuingia makubaliano ya kusaini mikataba ya kucheza pambano ili waweze kutambua afya zao.

"Mapromota mnapaswa kufahamu taarifa za afya za mabondia kabla ya kusaini mkataba, kwa sababu mchezo huu ni hatari," alisema Mwana FA na kuongeza:

"Jambo lingine ni bima za afya mabondia wanatakiwa kuwa nazo ili kupima afya kabla ya pambano na baada ya pambano ili kufahamu maendeleo yao."

Kwa upande wa Kaimu Mtendaji wa Baraza la Michezo la Taifa (BMT), Benson Chacha, alisema changamoto kubwa wanayoipitia kutoka kwa mapromota ni ucheleweshwaji wa vibali vya mapambano.

"Mapromota wengi wamekuwa na changamoto ya kuchelewesha vibali vya mapambano ya nje ya nchi," alisema Chacha.

Mwenyekiti wa TPBRC wa Kamati ya Mpito, Emmanuel Salehe, alisema walivyoingia katika uongozi waligundua kuwa makocha wengi hawana elimu ya mchezo huo.

Alisema wapo kwenye mchakato wa kumuita mkufunzi kutoka nchini Kenya kuja kuwapa elimu makocha ili kuendeleza mchezo huo.

"Tumeshafanya mazungumzo na mkufunzi huyo, hivi sasa tunasubiri kupata gharama zake ili tumtafute mdhamini ambaye atatusaidia ili kumleta hapa nchini," alisema Salehe.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### NAPOLI YAMTAKA RASHFORD
NAPOLI wanatarajiwa kuwasilisha ombi la kumnunua mshambuliaji wa Manchester United, Marcus Rashford mwenye umri wa miaka 27, huku winga wa Georgia, Khvicha Kvaratskhelia akitarajiwa kuondoka katika klabu hiyo ya Italia. (***Mirror***)

### KVARATSKHELIA HUYOOO PSG
KLABU ya Paris St-Germain inakaribia kumsajili Khvicha Kvaratskhelia kutoka Napoli, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, akiwa tayari ameshakubaliana maslahi binafsi na timu hiyo ya Ufaransa. (***Foot Mercato***)

### DURAN NAYE AKOMALIWA
PSG inaamini kuwa inaweza kuwashawishi Aston Villa kuwauzia mshambuliaji wa Colombia, Jhon Duran mwenye umri wa miaka 21, na klabu hiyo ya Ligue 1 ina nia ya kumjumuisha mshambuliaji wa Ufaransa, Randal Kolo Muani mwenye umri wa miaka 26, katika mazungumzo hayo. (***Mail***)

### ASENSIO SASA AGOMBEWA
KIUNGO mshambulizi wa Hispania, Marco Asensio mwenye umri wa miaka 28, anatarajiwa kuhama PSG, huku Aston Villa, Juventus na Real Sociedad zikitarajiwa kuwa mojawapo ya klabu anazoweza kujiunga nazo. (***Foot Mercato***)

### BARCA MACHO KWA ISAK
BARCELONA inamtaka mshambuliaji wa Newcastle United, Alexander Isak na inaweza kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, Januari hii au msimu wa majira ya joto, kulingana na hali yao ya kifedha. (***Mundo Deportivo***)

### WALKER ATAKIWA MILAN
AC Milan ina nia ya kumsajili beki wa England, Kyle Walker, huku Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola, akisema mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34. aliomba kuondoka katika klabu hiyo ya England. (***Guardian***)

### CHELSEA KUMKOSA GUEHI
MATUMAINI ya Chelsea ya kumsajili mlinzi wa England, Marc Guehi mwenye umri wa miaka 24, kutoka Crystal Palace huenda yakatibuka kwa sababu ya mfumo wa mshahara wa klabu hiyo ya Stamford Bridge. (***Mirror***)

### KROSCHE ANUKIA SOKONI
MKURUGENZI wa Michezo wa Eintracht Frankfurt, Markus Krosche, amethibitisha kuwa kuna klabu ambayo imewasiliana nao kuhusu usajili wa mshambuliaji wa Misri, Omar Marmoush. Manchester City walikuwa wameafikiana mkataba na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25. (***Sky Sports Germany***)

### ARAUJO KUBAKIZWA BARCA
BARCELONA imekataa ombi la Juventus la kumnunua beki wa Uruguay, Ronald Araujo na wanataka kumbakiza mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, ambaye mkataba wake na klabu hiyo ya Hispania unamalizika mwaka 2026. (***Mundo Deportivo***)

### CHUKWUEMEKA NA DORTMUND
KLABU ya Borussia Dortmund inafikiria kumsajili kiungo wa kati wa England, Carney Chukwuemeka mwenye umri wa miaka 21, kwa mkopo kutoka Chelsea. (***Sky Sports***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# GUARDIOLA: WALKER KAOMBA KUONDOKA MANCHETER CITY

**MANCHESTER,** England

●●●Amekuwa muhimu kwa timu yetu, lakini anataka kuangalia changamoto mpya, sijui nini kitatokea...

PEP Guardiola amefichua kuwa Kyle Walker ameomba kuondoka Manchester City.

Beki huyo wa England aliachwa nje ya kikosi kilichoshinda mabao 8-0 dhidi ya Salford City ya Ligi ya Daraja la Pili kwenye Kombe la FA Jumamosi.

Alipoulizwa baada ya mchezo kuhusu sababu ya Walker kuachwa, Guardiola alieleza kwamba Walker alimwomba Mkurugenzi wa Soka wa City, Txiki Begiristain, Alhamisi aruhusiwe kuhamia "nchi nyingine" katika dirisha hili la Januari.

"Si rahisi kwangu kusema kwa sababu ni lazima nimwambie, lakini hayupo, kwa hiyo siku mbili zilizopita Kyle aliomba kutafuta chaguzi za kucheza nje ya nchi mwezi huu," alisema Guardiola akiwaambia waandishi wa habari.

"Amekuwa beki wetu wa kulia, akitupa kitu ambacho hatukuwa nacho, lakini sasa akilini mwake angependa kuchunguza kwenda nchi nyingine kucheza miaka yake ya mwisho kwa sababu nyingi."

**Walker alikaribia kuondoka Etihad mwaka 2023 wakati Bayern Munich ilipompa ofa ya mkataba wa miaka miwili.**

Lakini alishawishika kubaki baada ya kufanya mazungumzo ya faragha na Guardiola na baadaye akasaini mkataba mpya wa miaka mitatu na kufanywa kuwa nahodha wa klabu.

Saudi Arabia inaonekana kuwa sehemu ambayo anaifikiria na hasa baada ya kuanza vibaya msimu na City, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, ambaye aliwasili kutoka Tottenham Hotspur 2017, amepoteza nafasi yake katika kikosi cha kwanza.

"Aliomba kuondoka miaka miwili iliyopita," alisema Guardiola.

"Bayern walimtaka lakini ofa haikuwa nzuri na klabu ilimwambia kwa namna alivyo muhimu. Hatuwezi kuelewa mafanikio tuliyopata miaka hii bila Kyle.

"Ninamheshimu sana kwa sababu nina shukrani zaidi tangu amekuwa hapa miaka mingi kwa ajili yetu. Msimu wake wa kwanza hapa, tulianza kushinda, kushinda, kushinda, kushinda na kushinda.

"Amekuwa muhimu kwa timu ya taifa na muhimu kwa timu yetu, lakini alisema kwamba 'nataka kuangalia changamoto mpya.' Sijui nini kitatokea."



# KVARATSKHELIA ANATAKA KUONDOKA NAPOLI - CONTE

**NAPLES,** Italia

KOCHA wa Napoli, Antonio Conte, amethibitisha kuwa Khvicha Kvaratskhelia ameomba kuondoka katika klabu hiyo huku kukiwa na nia ya kutakiwa na vinara wa Ligi Kuu England, Liverpool na viongozi wa Ligue 1, Paris Saint-Germain.

Kvaratskhelia, ambaye alishinda taji la Serie A akiwa na Napoli mwaka 2023, ana mkataba unaomalizika 2027, lakini amekataa kuongeza mpya msimu huu.

Akizungumza katika mkutano na waandishi wa habari kabla ya mchezo wa jana wa Napoli wa Serie A dhidi ya Verona, Conte alielezea masikitiko yake kuhusu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, kuwa huenda akawaacha mwezi huu.

"Sijawahi kujificha kutokana na maswali yasiyopendeza. Nikizungumza nitasema ukweli, vinginevyo napendelea kukaa kimya, sisemi uongo," alisema Conte.

"Tunazungumzia mchezaji muhimu ambaye tayari alitakiwa kuondoka majira ya kiangazi, pia nilitaka kuwa na uhakika wa kiufundi, ubora unahitajika pamoja na kazi niliyoitaka pamoja na uthibitisho wa baadhi ya wachezaji akiwamo Khvicha, ambaye, kama unavyojua, alikuwa ameomba kuuzwa katika majira ya joto na hakuwa peke yake.

"Tunasonga mbele, lakini ni rahisi kusahau kazi niliyopaswa kufanya ili kuwashawishi wachezaji, ambao niliwaona kuwa muhimu, kubaki. Wengi walitaka kuchukua njia nyingine.

"Aliomba klabu imuuze, bila kumung'unya maneno. Hiki ndicho nilichoambiwa, mchezaji huyo amethibitisha uamuzi wake kwangu.

"Binafsi ninahisi kukata tamaa sana, kwa sababu nilitumia miezi sita kujaribu kumfanya Kvaratskhelia ajisikie katikati ya mradi wangu, nikifanya naye kazi, nikimuonesha kwamba tunaweza kufanya kitu kikubwa na pia kufanya kazi na klabu kwa miezi sita zaidi.

"Leo lazima nirudi nyuma. Siwezi kuwaweka wale wanaotaka kuondoka wakiwa wamefungwa minyororo. Nilifanya hivyo majira ya joto na nikawa na miezi sita kushawishi pande zote kutafuta suluhu.

"Ninatambua kuwa habari hizi zimetoka nje, lakini sasa ninapiga hatua nyuma na ni sawa kwamba klabu na wasaidizi wa Kvaratskhelia wapo katika hatua ya kutatua hali hiyo."

# Pedri akanusha wachezaji Barca kuisusia Hispania

**JEDDAH,** Saudi Arabia

KIUNGO wa Barcelona, Pedri, amekanusha kuwa wachezaji wa klabu hiyo walifikiria kugomea kuichezea Timu ya Taifa ya Hispania kutokana na mzozo unaohusu usajili wa Dani Olmo.

Olmo na mchezaji mwenzake wa Barca, Pau Victor walipewa ahueni ya muda wiki hii, wakati Mahakama Kuu ya Michezo ya Hispania (CSD), inazingatia rufaa ya Barcelona dhidi ya uamuzi wa LaLiga na Shirikisho la Soka la Hispania kukataa usajili wao kwa nusu ya pili ya msimu.

Wachezaji wote wawili sasa wamesajiliwa tena wakati CSD ikichambua kesi hiyo, na walikuwapo kwenye kikosi cha Barcelona katika fainali ya Supercopa dhidi ya Real Madrid huko Jeddah, Saudi Arabia, jana Jumapili.

Kituo cha TV3 cha Katalunya kilisema kwamba wachezaji wa Kimataifa wa Barca walikuwa wakitishia kukataa kuichezea Hispania ikiwa usajili wa Olmo utakataliwa, wakipinga hatua ambayo pia ingemzuia kuiwakilisha nchi yake.



"Watu walisema wachezaji wa Timu ya Taifa ya Hispania hawataenda kucheza, lakini nilisikia hivyo na nilishangazwa na hilo, kwani huo ni uwongo," alisema Pedri katika mkutano na wandishi wa habari.

"Singekataa kuichezea timu ya taifa, napenda kuichezea timu ya taifa. Ni uongo, natumaini hakuna aliyeamini."

Sheria ya Hispania inawalazimu wachezaji wanaochaguliwa na timu ya taifa lazima wajiunge nayo.

Olmo na Victor waliondolewa kwenye usajili wa LaLiga Desemba 31 baada ya Barca kukosa vielelezo vya kuonesha kwamba wanaweza kuzingatia viwango vya matumizi ya kikosi cha ligi hiyo.

Klabu hiyo baadaye ilitoa uthibitisho unaohitajika, lakini LaLiga iligundua kuwa wachezaji hao hawakuweza kusajiliwa tena chini ya sheria za kupiga marufuku mchezaji kusajiliwa mara mbili na klabu moja katika msimu mmoja.

Barça ilikata rufaa dhidi ya uamuzi huo, na CSD kisha ikatoa zuio la muda kabla ya uamuzi huo.

"Ni habari njema kwetu," Pedri alisema. "Nafasi waliyokuwa nayo ni ngumu sana nikijua hawawezi kucheza, nina Dani Olmo kwenye meza yangu tunapokula, ni ngumu kusafiri huku bila kujua unaweza kucheza, nina furaha sana kwake na kwa Pau, bila shaka watachangia sana."

LaLiga imesema sasa inachunguza uamuzi wa CSD kabla ya kukata rufaa.

## Slot aukubali ukosoaji kwa Alexander-Arnold

**BARCELONA,** Hispania

KOCHA Mkuu wa Liverpool, Arne Slot, amesema ukosoaji ambao Trent Alexander-Arnold amekabiliana nao baada ya kiwango chake cha kukatisha tamaa dhidi ya Manchester United wiki iliyopita ni "pongezi" ya ubora wake na "kila mtu ana maoni" tofauti juu ya beki huyo.

Alexander-Arnold, ambaye mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu, ameanza kuchunguzwa wiki hii kutokana na uchezaji wake duni katika sare ya mabao 2-2 na timu ya kocha Ruben Amorim.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, alikuwa chini ya mpango wa Real Madrid mapema mwezi huu, ingawa ofa ya klabu hiyo ya Hispania ilikataliwa haraka na Liverpool.

Alexander-Arnold alijitokeza kwa njia ya kuvutia akitokea benchi katika kichapo cha Liverpool dhidi ya Tottenham Hotspur katikati ya wiki na kuvutia macho tena alipokuwa nahodha wa klabu yake hiyo ya utotoni iliposhinda mabao 4-0 dhidi ya Accrington Stanley katika raundi ya tatu ya Kombe la FA Jumamosi.

"Nadhani pongezi kubwa zaidi kwa Trent angeweza kupata majibu ya kila mtu baada ya mechi ya United," alisema Slot baada ya mechi.

"Kila mchezaji duniani, labda isipokuwa wachache, ana michezo mibaya na hiyo ni kawaida kabisa.

"Wakati Trent ana mchezo mbaya, kila mtu ana maoni yake juu yake. Labda hiyo ni kuhusiana na hali ya mkataba. Sijui kama hiyo haikuwzapo kama kila mtu angeitikia kwa njia sawa.

"Labda ni pongezi kubwa unayoweza kupata ikiwa umekuwa na nusu ya kwanza ya msimu na haujacheza mchezo mzuri dhidi ya United - na hiyo ilikuwa wazi kwangu, kwa mashabiki, kwa wachambuzi wote na wengi wao walikuwa wagumu kuelewa na labda hiyo ndiyo pongezi kubwa anayoweza kupata."

Kocha huyo wa Liverpool aliongeza: "Nafikiri ilikuwa vema kwake kucheza tena katika uwanja wetu wa nyumbani, ili kuhisi mapokezi kutoka kwa mashabiki tena, ambayo tayari yalikuwa mazuri tulipocheza na Tottenham Hotspur.

"Hilo pia lilikuwa maalum kwake leo. Hilo litamsaidia yeye na sisi tu kwa sababu ukitaka kufanya mambo maalum katika msimu, lazima tufanye kwa pamoja, si tu wachezaji na makocha bali na mashabiki pia."

## Wachezaji Simba watoa siri ya Fadlu

INATOKA UKURASA 24

huku kila mmoja akimpa jukumu lake la kufanya na si kwenda kucheza tu.

"Katika mchezo dhidi ya CS Sfaxien, kocha huyo alimpa kazi moja tu Elie Mpanzu, kumtuliza beki wa kulia, Salah Harabi, ambaye alionekana kuwa ndiye chanzo cha mashambulizi yote ya wapinzani wao nchini Tunisia.

"Tulipokuwa ugenini, kocha alimwambia Mpanzu, afanye kazi ya kumkimbiza beki huyo ili asiwe tena na hamu ya kupanda mbele kwa sababu alikuwa ndiye mtu hatari, anapanda kwa kasi, ana spidi na krosi za uhakika, wenyewe ndiyo walikuwa wanamtegemea kwenye mashambulizi, upande uliobaki wa Shomari Kapombe, Kibu Denis akaongezeka na Jean Ahoua ndiyo tukawa tunamtumia sisi kushambulia, tukawazima," alisema Ahmed.

## Simba hatari ndani ya boksi, Yanga nje balaa

INATOKA UKURASA 24

wa na mabao 22 iliyoyafunga karibu na lango.

Nafasi ya nne imechukuliwa na Singida Black Stars, ikifunga mabao 20, Fountain Gate ya tano na mabao 18, Tabora United ikishika nafasi ya sita, ikiwa na 16 ndani ya boksi, Coastal Union ya saba na mabao yake 14, huku nafasi ya nane ikichukuliwa na Dodoma Jiji, ambayo ina 13 iliyoyafunga ndani ya kisanduku cha hatari.

Kwenye mabao ya nje ya boksi, Yanga inaongoza pamoja na timu za Fountain Gate na Mashujaa FC, ambazo zote zimepachika mabao sita nje ya boksi kila moja.

Timu zinazofuatia ni Simba, Tabora United, Azam FC, JKT Tanzania na Kagera Sugar ambazo kila moja imefunga mabao matatu, wachezaji wake wakiwa nje ya eneo la hatari.

Takwimu zinaonesha kuwa mabao hayo 264, yamefungwa katika michezo 127 iliyochezwa mpaka sasa, ambapo mechi 94 zimetoa washindi na 33 zimeishia kwa sare.

Katika michezo 94 ambayo timu zimeshinda, mechi 58 timu zimepata ushindi zikicheza nyumbani na mechi 36 zimetoa washindi zikicheza ugenini.

# YANGA SC YATAJA SIKU YA KUTANGAZA USAJILI MPYA

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imesema kuwa itawatangaza wachezaji wake iliyowasajili kipindi hiki cha dirisha dogo, itakaporejea nchini kutoka Mauritania ambako jana usiku ilikuwa na kibarua cha mchezo wa Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi dhidi ya, Al Hilal Omdurman ya Sudan uliopigwa nchini Mauritania.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Ali Kamwe, alisema mipango yote ya usajili wa wachezaji wapya imekwenda vema na watawatangaza wakirejea nchini.

Klabu hiyo inahusishwa kumsajili winga Jonathan Ikangalombo, akitokea AS Vita Club ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, ikiwa pia imemsajili, Israel Mwenda, pamoja na wengine ambao itawatangaza.



Usajili mpya wa Yanga, Israel Patrick Mwenda, akiwa mazoezini hivi karibuni na wachezaji wenzake, hata hivyo, bado hajaingizwa rasmi kwenye mfumo wa usajili (TMS), licha ya kuanza kujifua na timu hiyo. Mwenda amejiunga na Yanga akitokea Singida Big Stars. **MPIGAPICHA WETU**

Kamwe alisema watakaporejea nchini kila kitu kitawekwa wazi na kuwaumbua wote ambao wanadai Yanga haiwezi kusajili mchezaji yeyote kwa sababu wanadaiwa.

"Wanasema Mwenda hawezi kucheza kwa sababu tunadaiwa, wakati anatakiwa apambane mwenyewe kuwania nafasi kwani eneo analocheza amekuta watu wanapiga kweli kweli, atacheza, lakini ni mpaka apambane," alisema.

Ikangalombo, alikuwapo jukwaani katika mchezo wa Ligi ya Mabingwa Afrika uliopigwa, Januari 4, mwaka huu, kati ya Yanga na TP Mazembe.

Ingawa Kamwe hajaongea lolote kuhusu mchezaji huyo, lakini ni mmoja wa wachezaji wanaotarajiwa kutambulishwa.

"Mmoja wa wachezaji tutakayemtambulisha anakimbia kama swala, na wengine wapo kutoka hapa hapa nyumbani tunawatambulisha," alisema.

**Desemba mwaka jana, FIFA ilitoa taarifa ya kuthibitisha kuwa Klabu ya Bechem United ya Ghana imeshinda kesi dhidi ya mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania, Yanga SC, kwa kushindwa kulipa dola 80,000 za Marekani kama ada ya usajili wa Augustine Okrah.**

Kwa mujibu wa barua hiyo, FIFA ikaipiga marufuku kufanya usajili hadi itakapolipa kiasi hicho. Aidha, Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), nalo liliagizwa kuweka marufuku ya usajili wa ndani kwa klabu hiyo.

Kabla ya hapo, aliyekuwa mchezaji wa timu hiyo, Okrah ashinda kesi yake dhidi ya klabu hiyo, ambapo ilifungiwa hadi watakapomlipa

Ilitakiwa kumlipa Dola za Kimarekani, 24,400 (zaidi ya milioni 66). Pamoja na faini ya FIFA Dola za Kimarekani, 3,000 (zaidi ya milioni nane).

Akizungumzia hilo, Kamwe alisema hakuna kitakachoizuia Yanga isisajili kwani inajua inachokifanya.

"Kila siku watu anasema tuna madeni, lakini tunasajili na watu wanachezaji, sisi tunajua tunachokifanya wala hatuna wasiwasi wote, tutakaowatangaza watacheza," alisema Kamwe.

# JKT Queens U-17 yapania ubingwa michuano GIFT

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa timu ya wasichana wenye umri chini ya miaka 17 ya JKT Queens, Ester Chabruma, amesema wamejipanga vema kupata pointi tatu katika mchezo wao wa leo dhidi ya City Lights FC ukiwa ni mwendelezo wa mashindano ya CAF U-17 ya Gift Girls Integrated Football Tournament (GIFT), yanayoendelea kwenye Uwanja wa Azam Complex uliopo Chamanzi, Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, kuelekea mchezo huo utakaopigwa leo majira ya saa 12:00 jioni, Chabruma alisema malengo yake ni kutwaa ubingwa wa mashindano hayo na kwamba wachezaji wake wote wana morali ya juu.

"Tumejipanga vema kuhakikisha tunaendeleza ushindani katika mchezo huo ambao ninaamini utakuwa mgumu na wenye upinzani mkubwa," alisema Chabruma.

Alisema hana wasiwasi na mchezo huo kwani amewaandaa vizuri wachezaji wake ili wapate ushindi katika mchezo huo.

Aidha, alisema anawashukuru mashabiki kutokana na ushirikiano mkubwa wanaowaonesha pindi timu yao inapokuwa inacheza.

Mpaka sasa JKT Queens inashika nafasi ya kwanza kwenye msimamo wa Kundi A ikiwa na pointi sita.

# Michezo

Jumatatu Januari 13, 2025

Nipashe





**Slot aukubali ukosoaji kwa Alexander-Arnold** UKURASA 22



Kikosi cha wachezaji wa Simba

# Wachezaji Simba watoa siri ya Fadlu

## ●●● Ni mkakati, uwazi na mbinu katika kuhakikisha wanapata matokeo, wasema...

**Na Adam Fungamwango**

HATIMAYE baadhi ya wachezaji wa Simba wametoa siri ya Kocha Mkuu wa timu hiyo, Fadlu Davids, kupenda kuwachezesha wote, badala ya kutegemea kundi la wachezaji fulani kikosini.

Wakiwa nchini Angola, wachezaji hao, Awesu Awesu na Kibu Denis, wamesema kocha Fadlu hupanga kikosi chake kutokana na aina ya wapinzani anaokwenda kucheza nao na si kila mchezaji anaweza kucheza kila aina ya mechi.

Wamesema kutokana na tabia yake hiyo, imewafanya wachezaji karibuni wote wawe wanapata nafasi ya kucheza kwa sababu kila mmoja ana kitu chake binafsi kinachompa faida kwenye aina fulani ya mchezo.

"Wachezaji wote tunamuonesha mwalimu ni kitu gani tunacho kwenye mazoezi. Ni sehemu ambayo kocha anaangalia kila aina ya kipaji, uwezo, upambanaji na kitu ambacho anaweza kumpa nafasi kwenye mechi.

"Baada ya hapo kuna mechi zinakuja ambazo anakuhitaji, zipo ambazo anasema kwa aina hii ya mechi hakuhitaji kwa hiyo unakuwa mvumilivu.

**"Anatuambia si kila mechi mchezaji anatakiwa acheze. Kila mechi ina aina yake ya uchezaji kulingana na mpinzani unayekwenda kucheza naye," alisema Awesu.**

Kwa upande wa Kibu alisema kocha huwa anawaambia kuna michezo anahitaji aina fulani za wachezaji na zingine hawahitaji.

"Anatuambia kuna mechi fulani namhitaji fulani na mchezo huu simtaki mtu fulani, ambaye hamhitaji anamwambia wewe utanisaidia kwenye mechi nyingine, hivyo unaendelea na mazoezi ili hata siku akija kukupa mchezo, ucheze kwa jinsi ulivyoagizwa na alivyokuona unafaa kucheza mchezo huo," alisema Kibu.

Fadlu, raia wa Afrika Kusini, aliyeichukua Simba kutoka kwa Abdelhak Benchikha raia wa Algeria, ameonekana kuwa mmoja wa makocha kivutio kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara kwa jinsi anavyowatumia wachezaji wake karibuni wote tofauti na watangulizi wake.

Kocha huyo amekuwa akiwachezesha wachezaji ambao hapo awali walionekana kuwa wameshuka viwango kwa makocha wengine.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema kocha Fadlu anawapanga wachezaji uwanjani

INAENDELEA UKURASA 23

## Simba hatari ndani ya boksi, Yanga nje balaa

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI jumla ya mabao 264 yakifungwa hadi kumalizika kwa mechi za mzunguko wa kwanza, Simba inaonekana ni hatari zaidi kufunga mabao wachezaji wake wanapokuwa ndani ya eneo la hatari, huku Yanga wakiwa nje ya boksi.

Kwa mujibu wa Kitengo cha Takwimu cha Dawati la Michezo la Nipashe, Simba inaongoza kwa kufunga mabao mengi ndani boksi, huku Yanga ikiongoza kwa mabao ya mbali.

Simba imepachika mabao 28 ndani ya eneo la hatari kati ya 31 ambayo imefunga mpaka sasa kwenye Ligi Kuu. Ni mabao matatu tu ambayo timu hiyo imefunga ikiwa nje ya boksi.

Watani zao wa jadi, Yanga wanafuatia kwa kufunga mabao ndani ya kisanduku cha hatari, wakipachika 26, huku Azam ikishika nafasi ya tatu, iki-

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >